

MASIHI

 Mwaweza kuketi. Kweli kunaonekana kama kuja nyumbani kurejea. Sisi, tukisikia huko nyuma kutoka kwa mchungaji wenu tena mambo ya ajabu ambayo Bwana amekuwa akifanya hapa kwenye kanisa la nyumbani tangu nilipokuwa hapa, alisema karibu mmekuwa na uamsho wa daima wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu. Loo, si ni ajabu kuufikia wakati wa Mungu, wakati ufaao tu? Kunatufanyia tu jambo fulani.

² Vema, tumekuwa na mmoja maskanini. Nilikuwa na mfululizo wa masomo, nilikuwa nikiwaambia, juu ya nyakati saba za mwisho za kanisa. Na, loo, jamani, nilipomalizia Jumapili iliyopita na mlango wa 4 wa Ufunuo:

³ Kusanyiko langu ni kama, dogo, yapata watu mia nne, ama mia tatu na hamsini, kitu kama hicho. Nami, nilipokuwa nikizungumza, na nilikuwa nimeitisha mstari wa maombi, na nikizungumza juu ya uakisi kutoka kwenye Utukufu wa Shekina hadi kwenye nyota—hadi kwenye nyota, hadi kwenye bahari ya kioo, ambapo dhabihu zilioshwa, mwajua, ambazo zinawakilisha wenye dhambi, maji ya farakano, basi nilipokuwa nikizungumza juu ya jambo hilo, kisha nikageuka kuwaombea wagonjwa, Malaika wa Bwana alishuka moja kwa moja mbele yao wote, akaenda moja kwa moja na kusimama pembeni pale, ndipo watu mia tatu au zaidi walisimama na kuiangalia kwa dakika kumi na tano, wakipiga mayowe, wakilia, na kumsifu Mungu; wote waliangalia. Mara ya kwanza alipokuja namna hiyo mbele ya kanisa letu, akaingia tu moja kwa moja, akasogea moja kwa moja pale, na kusimama pale.

⁴ Nikasema, “Mnaweza kuiona?” Kila mtu akaanza kupiga mayowe na kuanguka. Nayo Hiyo hapo, ile Nuru kubwa ya kaharabu ya Nguzo ya Moto, duara kamilifu kabisa, imesimama pale. Ndipo ikaanza kujitia Yenyewe uvuli, na kutia uvuli kila moja ya nyakati hizo za kanisa jinsi hasa nilivyokuwa nimewafundisha, katika ile Nguzo ya Moto. Mungu anajua hiyo ni kweli hapa mbele ya Biblia Yake. Yeye... Tunaishi katika wakati wa mwisho, hakika.

⁵ Loo, nina furaha sana kwamba nabii aliahidi ingekuwa Nuru jioni. Katika saa hii ambapo kuna giza sana ulimwenguni, na kujua ya kwamba tunaishi na kutembea katika Nuru, ile Nuru aliyoahidi, alisema angefanya hivyo, aliahidi angefanya, na sisi hapa, watu waliojaliwa usiku wa leo, kufurahia mambo hayo wakati wa mwisho.

⁶ Sasa, kumbukeni, Kanisa halitakuwa, halitakuwa kitu *kikuu*, kikuu, *kikubwa* mno. Daima, katika kila wakati, liko katika uchache tu, uchache tu... Na katika ule Wakati wa Giza

nusura lififie kabisa, halafu basi karibu lififie kabisa katika wakati huu hapa, kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia.

⁷ Ndugu Jack alinalika huko chini kuhubiri hizo nyakati saba za kanisa wakati mwingine, natumaini nitapata nafasi ya kufanya hivyo. Loo, hakika tulifurahia jambo hilo nyumbani. Jinsi Roho Mtakatifu alivyotubariki!

⁸ Na sasa tunaenda huko Beaumont kutoka hapa, na kuendelea hadi Pwani ya Magharibi, na kurudi na kuingia Ohio, kisha kushuka kupitia Virginia, na Carolina ya Kaskazini, turudi kutoka huko, twende Bloomington, Springfield, Chicago, kisha tuondoke huko, na kwenda kaskazini mwa British Columbia, Fort St. John, na Grande Prairie, Dawson Creek, na kupitia huko. Natumaini kurudi ifikapo Juni, Bwana akipenda, kuninii, hii ni miezi sita basi, nitarudi kwa wakati unaofaa kwenda ng'ambo, labda, Bwana akipenda, wakati huo.

⁹ Sasa, tuna furaha kuwa hapa usiku wa leo, na kuona wengi sana huko nje, na nyuso zinazong'ara, na mioyo iliyo wazi, na, ni wakati mzuri sana, sivyo? Tuko chini ya matarajio usiku wa leo, ndivyo nilivyo, ambayo Bwana atatujulisha, usiku wa leo, nguvu Zake na utukufu, atajionyesha Mwenyewe kwetu. Na afanye asifanye, basi tutamwamini vivyo hivyo tu.

¹⁰ Ndio kwanza nimwache maskini mwanamke mmoja akiya kutoka Ujerumani. Majuma machache yaliyopita, alipoteza mtoto mchanga. Naye alikuwa amesimama karibu na California, wakati mmoja, ambako walimleta huyo mtoto mchanga, aliyekuwa amekufa. Alikufa asubuhi moja yapata saa tisa ama kumi, wazazi walikuwa wameendesha gari siku nzima, na ilikuwa yapata saa tisa, kumi, kumi na moja, naam, yapata saa kumi na mbili alasiri, mama akiketi nyuma ya gari, ameshika maskini mwili huu baridi mikononi mwake. Basi walipofikia mahali nilipokuwa, San Bernardino, walimchukua mtoto huyo mchanga, wakamleta mahali nilipokuwa nimesimama, nami nikasema, "Loo! Mtoto amekuwa amekufa kwa muda gani?"

Akasema, "Tangu asubuhi ya leo, mapema."

¹¹ Ndipo nikauchukua maskini mwili huo, baridi, tayari ulikuwa umekakamaa, huku watu hawa wamesimama karibu, nikalishika mikononi mwangu, nikaanza kumwomba Bwana wetu wa thamani. Nikahisi mtoto alikuwa akipata joto, nikaendelea tu kumshika, katika dakika chache tu akaanza kurusha mateke, akilia, nikamkabidhi mama yake. Kwa hiyo, basi wakati. . .

¹² Sasa, mnaona, hatuyatangazi mambo hayo. Mnaona? Jambo ni kwamba, kuna madoido mengi—mengi kupita kiasi siku hizi katika ninii yetu. . . Tuna—tunajaribu kuwa na kitu *fulani* kikubwa kutangaza kitu fulani, la, si kwa ajili ya jambo hilo. Ulimwengu kamwe hautalipokea, hata hivyo. Yeye huja

Kanisani, ni kwa ajili ya Kanisa, wa—watu wa Mungu. Mambo haya makuu, ya madoido hayafai katika Ufalme wa Mungu.

¹³ Watu watashangaa watakapopata kujua waaminio ni akina nani, na ni nani wasio. Itakuwa kama ilivyokuwa wakati Yohana alipokuja, kule kuja kwa Yesu mara ya kwanza kulikuwa na Ana hekaluni, na Yohana Mbatizaji, na—na nanii, wachache tu ambao kweli walikuwa ni waaminio, kweli waliupokea. Sasa tunakutazamia kuja Kwake.

¹⁴ Maskini mama huyu aliyesimama pale, alikuwa, mtoto wake mchanga alifia huko Ujerumani, mumewe ni kasisi wa jeshi, nao wakapiga simu, ya kwenda mbali, yapata mara tano mchana na usiku kuniomba nije, walisema wanajua ya kwamba Mungu angemfufua mtoto huyo mchanga.

Nikasema, “Acheni niende nikaombe,” nami nikaenda na kuomba, nikaomba alasiri hiyo, usiku huo.

¹⁵ Nami nitawaonyesha kama madaktari wanaamini au la. Wakati tayari alikuwa amempa daktari kitabu changu asome, juu ya, ninaamini, kinachoitwa *Nabii Azuru Afrika*, kitu kama hicho, na wakati. . . Akasema, “Mungu atamfufua huyo mtoto,” maskini mama huyo akasema, “Mungu atamfufua huyo mtoto mchanga.” Naye huyo mtoto alikuwa amekufa kabla hawajajua, yapata saa nne ama tano. Na kwa hiyo, wakampasha huyo baba habari, huko chini kwenye kituo alimokuwa. Naye huyo mtoto alikuwa amekufa, alikufa usiku.

¹⁶ Na kwa hiyo, daktari akasema, “Vema. Hebu niwaambie nitakalofanya,” kasema, “Nitaingia kisiri na kuifungulia oksijeni tena.” Naye akamwacha mtoto huyo alale pale kwa siku mbili huku oksijeni imefunguliwa, akingojea. Nami nilikuwa hapa nikiomba, walikuwa wanirushe kwa ndege, ningeweza kuondoka hapa kwa ndege ya Jeshi na nirudi siku iyo hiyo, hadi Ujerumani.

¹⁷ Ndipo asubuhi moja yapata mapambazuko nikaamka, naye mke akatoka humo chumbani, alipotoka chumbani, ndiyo kwanza niamke, nami, nikiwa nimelala pale kidogo, mara nikasikia Kitu fulani kikiingia chumbani, ndipo nikaangalia, kulikuwa na kitu Fulani kikitembea chumbani. Nami nikaruka tu juu, na kusema, “Bwana, ungetaka mtumishi Wako ajue nini?”

Kasema, “Usiukemee huo, huo ni mkono wa Bwana.” Mnaona?

Kwa hiyo nikampata kwa simu, nikasema, “La, Mungu amemwita mtoto wako.”

¹⁸ Na kwa hiyo, alipokuja huku kutuona, usiku ule, nilimwacha nyumbani nilipoondoka jana, akasema, “Ilikuwa ni nini, Ndugu Branham? Udhaifu wa—wangu wa imani?”

¹⁹ Nikasema, “Una imani kuu, ulimwomba mtoto wako mchanga, wewe na mume wako mlilikilia kwa Mungu,

kumfufua mtoto huyo mchanga, Naye akakataa kufanya hivyo kwa sababu anajua kilicho bora zaidi, nanyi mngali mnampenda.”

²⁰ Hiyo ni imani halisi. Mtu yeyote, wakati milima inaposogea, na kadhalika, anaweza kuwa na imani, lakini acha irudi nyuma wakati mmoja, uone jinsi inavyofanya kazi, hapo ndipo unapothibitisha kama una imani au huna.

²¹ “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kurudiwa na kujaribiwa na Mungu.” Kwa hiyo kumbukeni, majaribu yetu huleta saburi, nayo saburi huleta tumaini, na kadhalika. Kwa hiyo tunashikilia tu kwa Mungu, kama Yeye anatubariki au la, tuko papo hapo kumwamini Yeye kwa vyovyote vile, maana Yeye ameahidi hilo. Na kuona jinsi Yeye afanyavyo!

²² Sasa, kabla hatujaliandea somo kwa kusomwa kwa Neno, kwa sababu imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu... Na sasa, sitaki kuchukua muda mrefu kupita kiasi, maana Ndugu Jack wakati aliponipigia simu na kuniomba nipitie huku, ambalo nilifurahia kufanya, alisema walikuwa na wagonjwa wengine waliotaka kuombewa. Vema sana, tuliwazia tungefanya hivyo, kisha tuzungumze nanyi muda kidogo kabla hatujawaomba wagonjwa.

²³ Basi nilimtuma Billy usiku wa leo, alisema alisambaza kadi za maombi, ili kwamba kama kulikuwa na umati mkubwa, uliosongamana, vema, tungewaita kutokana na kadi za maombi, wala sio, sio lazima tuwe nazo.

²⁴ Kwa hiyo, kabla hatujalikaribia Neno Lake, hebu na tumkaribie Yeye kwa muda mfupi tu wa maombi. Kuna yeyote angependa kukumbukwa katika maombi haya usiku wa leo? Mungu awabariki. Mungu na ayajibu maombi yako, Yeye anajua mahitaji yako.

²⁵ Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, sijui kama kuna mwanamume mwenye dhambi, ama mwanamke, mvulana, ama msichana angetaka kusema, “Nikumbuke, Ndugu Branham, mbele za Mungu, usiku wa leo, unapoomba.” Waweza kuinua mkono wako? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Wengi, kote jengoni, yapata mikono kumi ama kumi na mitano imeinuliwa, wenye dhambi.

²⁶ Wengine wasio na Nuru ya Mungu nafsini mwao kwa Roho Mtakatifu, waweza kuinua mkono wako? Useme, “Nikumbuke, Ndugu Branham.” Mungu akubariki. Loo, mikono tu kila mahali.

²⁷ Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia kiti Chako cha neema na rehema. Tunakuja, kwa unyenyekevu, katika Jina la Yesu kwa sababu tuna hakika ya kwamba Yeye atatusikia, kwa kuwa Yeye alisema, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Basi hiyo ndiyo ahadi, kwamba tunajua hiyo ni kweli, haidhuru jinsi kutokuamini kwetu kunavyoizua, hata

hivyo ni kweli. Kwa hiyo tunaamini, usiku wa leo, kwa yote yaliyo ndani yetu, kwamba Wewe unatusikia.

²⁸ Tunaamini ya kwamba Wewe upo hapa, na utayajibu maombi yetu, na hasa kwa wale wenye dhambi walioinua mikono yao, jalia waione Nuru ya Mungu, usiku wa leo. Jalia madhabahu hii iwakute wamelala kifudifudi juu yake, wakiomba rehema kwa ajili ya nafsi yao yenye dhambi. Tujalie, Bwana.

²⁹ Ninawaombea wale ambao hawana Roho Mtakatifu maishani mwao kuwaongoza. Mungu na aingie kwenye mnara huo wa kuongozea usiku wa leo na kuchukua mamlaka, akiongoza Nuru yao, maisha yao katika saa hii yenye giza, inapofikia wakati ambapo mataifa hayajui la kufanya, bali Wewe ndiwe Njia, Kweli, na Uzima. Tuna furaha sana kwamba tuliwahi kukuona Wewe, Bwana, miaka mingi iliyopita, wa thamani sana moyoni mwetu, Wewe ni Msaada upatikanao wakati wa shida. Ninawaombea, kila mmoja, ya kwamba watajazwa na Roho Mtakatifu, usiku wa leo.

³⁰ Wabariki wagonjwa na wanaoteseka walio katika hili jengo na nje ya jengo, wakipata nafuu, ama popote walipo, tunawaombea rehema, Baba.

³¹ Sasa, tungekuomba Wewe ulibariki kanisa, uendeleo kulibariki. Tunataka kukushukuru kwa yale unayolifanyia kundi hili la mahali hapa, hapa, la waaminio, hawa watu watakatifu, watawa wanaolicha Jina Lako, Bwana, na kuamini ya kwamba utakuja, siku moja, kutupokea. Tujapolala mavumbini, halitatuzuia, kwa maana parapanda ya Mungu Italia, waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza, tunaenda, kwa vyovyote vile, mauti hayawezi kutuzuia, hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kukutana Naye.

³² Ee Mungu, tuna furaha sana kuwa na Damu ya Yesu iliyopakwa nafsi mwetu, Roho Wake akiishi ndani yetu! Tunaomba sasa ya kwamba utamfanya kila mmoja wetu raia wa Ufalme, usiku wa leo. Mungu, waponye wagonjwa na wanaoteseka, jipatie Mwenyewe utukufu.

³³ Na tunapolikaribia Neno Lako sasa kwa ajili ya ujumbe kwa kusanyiko hili linalongojea, wengine wakingojea kubarikiwa, wengine wakingojea kujazwa, wengine wakingojea kuponywa, wengine wakingojea kuokolewa, jalia Roho Mtakatifu ahudumie kila mmoja wetu, Bwana, kulingana na mahitaji yetu.

³⁴ Na haja yangu, kwa kilindi, ni sasa, Bwana, ni Wewe, uje ukanene, Ee Mungu, na ujalie Roho Mtakatifu atende kazi juu ya Neno kama alivyotembea juu ya maji hapo mwanzo, na kusema, "Iwe Nuru," Neno linapoendelea, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

³⁵ Katika somo, kama ungetaka kulitia alama...Nami nimezoa, majuma machache yaliyopita, kunena na kutia alama

sehemu za Maandiko, nami nina karibu kurasa nne zake hapa, sijui jinsi ningepata kuzifikia. Lakini, kama ungetaka kufanya hivyo, mbona, unakaribishwa hata na zaidi. Nafikiri wakati mwingine sasa kwa kuwa mwisho umekaribia sana, niliwazia, labda, ningefundisha tu kidogo juu ya somo fulani.

³⁶ Mwaweza kufungua Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza. Nasi tunganisoma Andiko la kwanza kutoka kwenye mlango wa kwanza, na somo la pili la Maandiko kutoka kwenye mlango wa 4 wa Yohana Mtakatifu. Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, na kifungu cha 40 cha mlango wa kwanza, tusome hadi cha 43. Na mlango wa 4, tunaanzia kwenye kifungu cha 24, cha 25, na cha 26. Mlango wa kwanza, kifungu cha 40:

Andrea, nduguye Simoni Petro, alikuwa mmoja wa wale wawili waliomsikia Yohana na wakamfuata Yesu.

Huyo akamwona kwanza Simoni, ndugu yake mwenyewe, akamwambia, Tumemwona Masihi, ambayo ni, ikifasiriwa, Kristo.

Naye akamleta kwa Yesu. Naye Yesu akamtazama, akasema, Wewe ni Simoni, mwana wa Yona: nawe utaitwa Kefa, tafsiri yake, Jiwe.

³⁷ Na katika kifungu cha 24 cha mlango wa 4 tunasoma hivi:

Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kutwabudu katika roho na kweli.

Yule mwanamke akamwambia, Najua ya kuwa yuja Masihi, aitwaye Kristo: naye atakapokuja, yeye atuatambia mambo yote.

Yesu akamwambia, Mimi ninayesema nawe, ndiye.

³⁸ Ninataka kuchukua neno lenye herufi tano kutoka hapo kwa ajili ya somo: M-a-s-i-h-i, *Masihi*.

³⁹ Ninataka somo langu usiku wa leo liwe kwenye neno *Masihi*. Neno lenyewe linamaanisha “aliyetiwa Mafuta,” au lingeweza kutumiwa “Mfalme aliyetiwa Mafuta,” na pia linamaanisha “Kristo.” Lakini tutalitumia kwanza katika wazo hili la “Mfalme aliyetiwa Mafuta.”

⁴⁰ Linaonekana kwanza katika Mwanzo 3:15, kama ukitaka kuandika Maandiko, yule Uzao aliyeahidiwa wa mwanamke, ambaye alikuwa awe Ndiye mtiwa Mafuta. Kote katika Maandiko manabii wote hunena juu ya Yule ajaye, yule Mfalme aliyetiwa Mafuta. Ninapenda hilo neno *mtiwa mafuta*, Mungu akimtia mafuta Mmoja. Naye alikuwa awe Mfalme ambaye atawaweka huru Israeli kutoka kwa mataifa yote, na kuwafanya wayatawale mataifa, Mfalme aliyetiwa Mafuta alipaswa kufanya hivyo.

⁴¹ Ninaamini ya kwamba Yesu wa Nazareti alitimiza kila sifa ambayo manabii wote walinena kwamba ni Masihi. Ninaamini

ya kwamba katika Isaya 9:6, wakati ninii, walipokuwa, Israeli walipokuwa wameomba ishara, Mungu alisema, “Nitawapa ishara ya milele,” ishara, ishara ya Milele, moja ambayo ingekuwa milele, kasema, “bikira atachukua mimba, hiyo itakuwa ni ishara. Na Yule atakayezaliwa naye, ataitwa Jina Lake, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, na Baba wa milele.” Nami ninaamini ya kwamba Yesu alitimiza kila maelezo ya kila ahadi ambayo Yehova alitoa kama Mfalme na Masihi ajaye.

⁴² Haidhuru jinsi wengi waliamini pakubwa kwamba Yeye alishindwa vibaya sana katika kazi Yake, Yeye angali ni Mfalme, Yeye ni Mfalme sasa, Yeye ni Mfalme wa watakatifu, Ufunuo unasema hivyo, “Ewe Mfalme wa watakatifu.” Anao Ufalme. Hivi huna furaha wewe ni wa Utawala huo usiku wa leo, katika Utawala wa Mtiwa Mafuta? Isitoshe, bali ametufanya wafalme na makuhani kwa Mungu, waliotiwa mafuta kwa Mungu.

⁴³ Sasa, ingawa Yesu, akitimiza masharti haya yote, nao Wayahudi walikuwa wamesoma ahadi hizi kwa miaka mingi, liliwapitaje, na kuponyoka bila wao kuliona? Hao wanatheolojia, waliosoma Maandiko vizuri sana, wanaoyashika sana Maandiko yao, na hata hivyo wakashindwa kumwona Yeye kuwa Ndiye aliyetiwa mafuta. Inasikika ingawa isingetendeka, inaonekana kana kwamba wangalimjua Yeye, wajuji sana, lakini Mungu aliyapofusha macho yao.

⁴⁴ Inaonyesha ya kwamba ulikuwa ni mkono wa Mungu. Yeye alijulikana dhahiri mno, ishara Zake za Masihi zilimthibitisha kuwa Masihi, zikamthibitisha kuwa Ndiye aliyetiwa mafuta. Nao kulikosa, hakika ilibidi uwe ni mkono wa Mungu kuwapofusha, kwamba hawakulikosa, ama kwamba wao, ama ambapo wasingalilikosa, hasa. Na ni jambo lile lile siku hizi, kama Injili imefichwa, imefichwa kwa hao walio vipofu, na njia pekee wanayoweza kupata kuona ni kupitia kwa Mungu.

⁴⁵ Sasa, Isaya 9:6, kamwe hatutaisoma, bali Yeye alikuwa awe Baba wa milele, Mungu Mwenye Nguvu. Wakati Mungu alipomfanya mtu katika Mwanzo 1:26, inaonyesha, kama mnayaandika Maandiko hayo, Mwanzo 1:26, inaonyesha ya kwamba kwanza kabisa Mungu alimfanya mwanadamu kuwa mungu mdogo, mwanadamu alifanywa kuwa mungu, mungu mdogo. Yeye aliumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, alikuwa na mikono kama ya Mungu, alikuwa na miguu kama ya Mungu, macho, masikio, na akili kama Mungu, umbo lake lote, kwa sababu alikuwa ni mwana wa Mungu, na, Yesu alimtaja kama mungu.

⁴⁶ Yesu alisema, “Mnawezaje kunihukumu Mimi nikisema Mimi ni Mwana wa Mungu? Haikuandikwa katika torati yenu ya kwamba ninyi ni miungu? Na kama wanawaita hao miungu, ambao walijiliwa na Neno la Mungu, mnawezaje kunihukumu

ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?” Alikuwa akiwarejea manabii, waliotiwa mafuta, walio na upako mdogo. Yesu alikuwa ametiwa mafuta sana hata alikuwa ni zaidi ya nabii, Yesu alikuwa ametiwa mafuta sana hata alikuwa ni Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, Yeye *alikuwa* ni Mungu. Manabii walikuwa na upako wa aina ile ile, ila tu katika hali ya chini.

⁴⁷ Na katika Mwanzo 1:26, wakati Mungu alipomfanya mtu, Yeye alimfanya mungu, kwa sababu alimpa milki, na alikuwa na utawala. Alikuwa na mamlaka juu ya ndege wa angani, wanyama, juu ya pepo, mawimbi, sa—samaki wa baharini, ninii, kila kitu, alikuwa na mamlaka juu ya kila kitu. Alikuwa mtawala, mtawala aliyetiwa mafuta, kwa sababu alikuwa katika mfano na katika sura ya Mungu akiwa na milki ya duniani. Hiyo ndiyo sababu Biblia inasema dunia inaogua, inalia, ikingojea, kule kudhihirishwa kwa wana wa Mungu, ulimwengu unamngojea mtu huyo kurudi katika urithi wake halisi.

⁴⁸ Sasa, yeye amefanywa katika mfano na sura ya Mungu, hiyo inafanya ninii yake. . . Wakati Mungu alipomwumba, Mungu alimpa Roho Yake kidogo, sehemu ya Uhai Wake, naye yuko katika mfano na sura ya Mungu. Kwa hiyo kama hapa katika ninii, mwanadamu katika hali yake ya kawaida, jinsi tulivyo sasa, mnaweza kuona ya kwamba yeye ni zaidi sana ya mnyama, kama wanavyojaribu kusema ndivyo tulivyo, kwa sababu mwanadamu, katika hali yake ya kuanguka, hata hivyo akiwa ni mwana wa Mungu aliyeanguka, angali anaweza kujiboresha, ana akili.

⁴⁹ Yeye hujijengea nyumba bora, hali za maisha; anajitengenezea hali bora za usafiri, anaweza kwenda kasi sasa hewani kwa mwendo wa maili elfu moja mia tisa kwa saa kwa ndege, ama roketi.

⁵⁰ Naye ame—amejizatiti hata karibu aweze kuuzunguka ulimwenguni katika saa ishirini na nne tu, kutuma tu se—setilaiti hewani juu ya anga ya mahali ambapo hewa inapinduka, mzingo wa dunia, na kusimama kimya, na kuuangalia ulimwengu ukipita chini yake, na kuzunguka kabisa katika saa ishirini na nne, huku amesimama kimya tu mahali pamoja, aende juu hewani na kusimama kule, anarudi moja kwa moja chini, na kuwa nyumbani tena, akisimama tu juu ya—ya dunia inayozunguka, ambapo dunia inavuta mkondo wake pande zote, ikifanya upepo, na kadhalika, mkondo.

⁵¹ Ulimwengu ukizunguka, karibu maili elfu mbili mia tano kwa saa, la, nitasema yapata maili elfu moja mia moja kwa saa. Ni maili elfu mbili mia tano kuizunguka, na inazunguka kila saa ishirini na nne, inakuwa karibu maili elfu moja mia moja kwa saa. Naye anapanda juu hewani, na kuasi hizo, anasimama juu ya nguvu za uvutano, na kusimama huko na kuangalia ulimwengu ukipita chini yake. Yeye ni mwerevu, mwenye akili. Naye a—

ameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, na ndani yake kuna Nuru.

⁵² Sasa, kwa mfano wakati mtu anapookoka, yeye ni kama tu. . . Nuru inayoingia ndani yake ni kama kifungo hiki kidogo cheupe kwenye shati langu. Hapo ni wakati Mungu anapoingia katika sehemu ya ndani ya mtu. Katika sehemu ya ndani ya mtu ama. . . Mtu ameumbwa katika mfumo wa maskani, katika nyua za nje, halafu mahali patakatifu, na Patakatifu pa patakatifu, Utukufu wa Shekina ndani, lile pazia.

⁵³ Sasa, kwenye malango ya nje ya mtu kuna hisi zake tano zinazolingia mwilini mwake. Ndani, ambayo ni nafsi yake, ama, na—na—nafsi ndiyo asili ya roho iliyo ndani ya moyo wake, hutoa nafsi yake, ambayo hufanya mazingira yanayomzunguka, pia ana milango mitano.

⁵⁴ Halafu upande wa ndani, ana lango moja tu, mlango mmoja wa kuingia katika Utukufu wa Shekina, ambapo Mungu anaweza kuingia ndani yake, na kuudhibiti mnara wa kuongozea. Na njia hiyo ni kupitia kwa hiari. Kama unataka, au hutaki, hiyo ni juu yako. Lakini hiyo ndiyo njia pekee iliyo wazi kwa huyo mtu ambayo Mungu anaweza kuingia moyoni mwake, ni kwa hiari yake mwenyewe. Inamrudisha moja kwa moja kama Adamu na Hawa kwenye uhuru wa kujichagulia tena. Unaweza kuchagua mema au mabaya, mojawapo utakayo.

⁵⁵ Sasa, hiari, ndipo Mungu anaingia ndani ya mtu, ndani ya moyo, ambao ni roho, kisha roho inaifanya nafsi, ndiposa nafsi inakaa katika huo mwili. Sasa, mtu anapoongoka, tuseme, kama tu kile Kifungo kidogo cheupe kinavyoanza moyoni mwake, sasa, sehemu hiyo ni Mungu, Mungu, wakati mtu anapozaliwa mara ya pili na Roho wa Mungu, Roho wa Mungu anakaa ndani yake.

⁵⁶ Sasa, kwa kuwa anaweza kumwacha Roho huyo akue, na kuondoa mizizi yote ya uchungu, na kusukuma njia ya Mungu kupitia kwake tena, anaweza kurudi katika hali ile ile aliyokuwamo wakati alipokuwa katika bustani ya Edeni. Yesu alisema katika—katika Marko 11:24, “Amin, amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka, wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Hilo linamrudisha moja kwa moja kwenye hali ya juu sana tena, linamrudisha moja kwa moja katika hali hiyo.

⁵⁷ Sasa, tumeumbwa kwa vipimo vya nuru, ndani yetu kuna nurulimwengu. Sasa, hiyo nurulimwengu ni nuru ambayo wanaweza kupiga picha ya eksirei nayo. Eksirei haitoki kwenye nuru ya eksirei, inatoka kwenye nuru yako mwenyewe. Na halafu kama hiyo nurulimwengu, tuseme, ingeweza kusukumwa mahali ambapo si nurulimwengu, bali Nuru ya Milele, Mungu angeweza kuchukua mamlaka yote, awaze kwa niaba yetu, atembea kwa niaba yetu, azungumze kwa niaba yetu, basi si huyo mtu tena, ni Mungu ndani ya huyo mtu.

58 Nadhani ninawaziba masikio kwa kitu *hiki*, maana ninakisikia kikirudisha mwangwi, kina sauti mbaya sana. Si mimi, ni *hiki*, sasa mnaona, kilaumuni hicho.

59 Sasa, yeye ana Nuru, Uzima. Uzima wa Milele ni Nuru ya Mungu inayokaa ndani ya mtu. Na kadiri atakavyojitolea kwa Roho, ndivyo anavyozidi kujiondolea ubinadamu -kuwa kama mwenye dhambi, na anakuwa zaidi kama Mungu.

60 Hapa si muda mrefu uliopita walipiga picha ya eksirei ya mtu fulani akimwomba mgonjwa, *Reader's Digest* iliandika, wakaona mwali wa Nuru ukitoka kwa mmoja wa hao watu, sio wote, lakini mmoja wa mikono ya watu hao uliakisi mwali wa Nuru walipoweka kipande cha karatasi ya risasi chini ya mkono wa huyu mtu. Nadhani ulisoma hilo wewe mwenyewe.

61 Huko Uingereza, waliwaachilia *waponyaji*, walivyowaita, kwenye hospitali zote, kulikuwa na asilimia themanini zaidi ya uponyaji uliofanywa kwa uponyaji wa Kiungu kuliko tiba za kidaktari zilivyokuwa zimefanya. *Reader's Digest* iliandika hilo hapa, hayo yalikuwa katika *Newsweek*, nayo *Reader's Digest* ikalichukua na kulifanyia uchunguzi, nao wakagundua kwamba kuna mwali wa Nuru.

62 Wakati mtu huyu, kwa unyofu, bila kujua walikuwa wakifanya hivyo, alipomwekea mikono mtu fulani na kuomba maombi ya bidii, walikuwa wakiweka eksirei chini, ndipo wakaona Nuru, ikitoka mkononi mwake. Mungu alijua yale aliyozungumzia aliposema, “Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Anajua alichokuwa akizungumzia. Loo, ninataka kuona Kanisa likisonga liingie mahali pale ambapo linaweza kufanyika jinsi Mungu anavyotaka liwe!

63 Ndipo Mungu alipofanyika mwili na akawa Masihi, basi kama tunaweza kujitolea tutiwe mafuta kama Yeye alivyokuwa, tunakuwa Masihi wadogo, Nuru ndogo ndogo. Hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuwa, Nuru, watiwa mafuta wadogo. Hilo ni Kanisa la Mungu.

64 Nuru Yake inayosimama ni Nuru ya Masihi, Kristo aliyefufuka ndani ya watu Wake, watiwa mafuta, akiipeleka Nuru Yake katika nyakati zote za kanisa. Wakati mwingine inakaribia kuzima kabisa, kisha inarudi tena, Mtiwa mafuta wa Mungu, Kanisa la Mungu la Kimasihi.

65 Kama *Masihi* linamaanisha “Mtiwa mafuta,” na linamaanisha “Mfalme,” basi kama Kanisa limetiwa mafuta na Roho wa Masihi, linakuwa wa kiwango kidogo, lakini hata hivyo, ni Masihi, kwa sababu lina Nuru Yake, likiakisi nguvu Zake, likiakisi utukufu Wake, likiakisi utawala Wake, kwa hiyo ni *Masihi*. Loo, jinsi linavyomwakisi katika Ufalme Wake katika milki Yake!

⁶⁶ Shida siku hizi, tumeliundia kanisa dhehebu hata kufa, nasi tuna madhehebu badala ya Nuru ya Masihi. Tuna Waruseli, waongofu, na *nuru* za aina zingine zote, bali tunahitaji *Nuru* ya Masihi, kile kanisa linachohitaji siku hizi, *Nuru* ya Masihi. Loo, ninampenda kwa ajili ya wema Wake!

⁶⁷ Sasa, hiyo ni kweli, Mungu aliwaita Masihi, Mungu alituita, nasi tunakuwa wafalme na makuhani kwa Mungu, kama vile Yesu alivyokuwa Kuhani Mkuu wa Mungu, tunakuwa kuhani mdogo. Yesu alikuwa ni Mungu katika Utimilifu, aliishi ndani Yake apate kuangaza dhihirisho la Mungu kwa ulimwengu, kwa kuwa Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Na kama vile Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake, Mungu anaingia ndani ya Kanisa Lake na kuwatia baadhi ya Masihi wadogo mafuta. Loo, jamani! Mnaliona?

⁶⁸ Mambo yale yale aliyofanya yako katika Kanisa Lake, nguvu zile zile alizokuwa nazo ziko katika Kanisa Lake, nalo Kanisa Lake linakuwa Milki Yake, Naye ni Mfalme juu ya Milki hii, nasi ni wafalme na makuhani, tukimtolea Mungu dhabihu za kiroho, matunda ya midomo yetu tukilisifu Jina Lake. Amina. Loo, jamani! Haya basi. Masihi wadogo, Masihi wadogo, masihi wadogo, watiwa mafuta wadogo. Waliotiwa mafuta kutokana na nini? Yule mkuu, wametiwa mafuta kutoka kwa Yule aliye mkuu.

⁶⁹ Loo, wakati Yesu alipokuwa duniani, wasingeweza kukana kwamba Yeye ni Masihi, kwa sababu alifanya ishara za Masihi. Wayahudi walipofushwa, na hiyo ndiyo sababu hawakumwona na kuona ishara Zake kama Masihi. Hiyo ndiyo shida ya kanisa usiku wa leo, limepofushwa, ulimwengu wa nje, hawawezi kuliona, kwa sababu mungu wa dunia hii ameyapofusha macho yao yasione mambo ya kiroho. Loo, laiti tungaliweza kuelewa!

⁷⁰ Yesu alienda kila mahali na kufanya ishara za Masihi, nao watu wakamkufuru. Na kama walimkufuru Mfalme mkuu aliyetiwa Mafuta, Masihi, ni zaidi sana vipi watawaita wale wa nyumbani Mwake, wa Ufalme Wake? Beelzebuli, na chochote kile walichomwita, wanawaita mabaya kuliko hilo, “Mtakatifu anayejibingirisha, mtakatifu arukaye, *kitu kingine*.” Daima wana jina la kashfa kwa ajili Yake, kwa sababu linatoka kwa ibilisi. Nao wakawaita watu wa nyumbani Mwake, Yeye alisema, kuliko yale wao . . . kama walimwita hivyo, wangewaitaje watu wa nyumbani Mwake? Lakini hata hivyo, ni mambo ya tu.

⁷¹ Sasa unasema, “Sasa, Ndugu Branham, Yesu alikuwa na ishara ya Masihi. Tunajuaje hiyo ishara ilikuwa nini?” Vema, wakati Yeye alipokuja, Biblia ilisema ya kwamba atakapokuja Masihi, Yeye angekuwa Na—Nabii, naye angeonyesha ishara za nabii, mwalimu yeyote wa Maandiko anajua hilo, Musa alisema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.”

⁷² Nao hao, wakati alipofanya ishara hizo za kujionyesha Mwenyewe, kama katika ninii—mlango wa 4 hapa, alipomwambia yule mwanamke alikuwa na waume watano, yeye alisema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba Masihi atakapokuja, Yeye atatuambia mambo yote.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

Akakimbia mjini na kuwaambia watu wote wa mjini, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

⁷³ Yesu alisema, Mwenyewe, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Kama ninadai kuwa na upako, wala sifanyi kazi za Mungu, maana nimetiwa mafuta Naye, pamoja Naye, si Mimi nizitendaye hizo kazi, hiyo ni kusema, Baba anayeishi ndani Yangu, Yeye huzitenda hizo kazi, na kama sizitendi hizo kazi, basi msiniamini Mimi, bali nikizitenda, ziaminini.”

⁷⁴ Sasa, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya Masihi, kwa Masihi wadogo, Kanisa. Hili hapa linakuja. Mko tayari? Yohana Mtakatifu 14:12, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya,” Masihi wadogo, hiyo ni kweli, Masihi wadogo, uwakilishi wa Masihi duniani, bado.

⁷⁵ Marko 16, Yeye alisema, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana,” na Masihi wadogo. “Aaminie na kubatizwa ataokoka. Yeye asiyeamini atahukumika, na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

⁷⁶ Umbali gani? Kwa ulimwengu wote. Kwa nani? Kila kiumbe. Loo, nina furaha sana! Utalifutulia mbali vipi hilo?

Kasema, “Ni kwa wanafunzi tu.”

⁷⁷ Ati kwa wanafunzi? Alisema, “Ulimwenguni kote, na kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

⁷⁸ Nashangaa ambapo watu ambao hawaamini katika ishara na maajabu kuwafuata waaminio, ungewezaje kusoma historia ya kanisa na kuwazia zilikoma na mitume? Nyakati za kanisa, nilisoma Wazee wa Nikea, *Baraza la Nikea*, loo, waandishi wote wa kale nilioweza kuwazia kusoma, *Babeli Mbili* cha Hislop, na vingine vingi vya vitabu vya kale, na kote kote hata kwenye kanisa Katoliki la mwanzoni, mpaka kufikia miaka mia sita ya kwanza baada ya Kristo, kulikuwako na Ireneo, Mtakatifu Martin, Columba, na hao wote, kila mmoja wa hao watu watakatifu, walihubiri ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, walihubiri ondoleo la dhambi, walihubiri kunena kwa lugha, wakawafufua wafu, wakawaponya wagonjwa, ishara na maajabu ziliwafuata moja kwa moja hata kwenye zile Nyakati za Giza, na kupitia hizo Nyakati za Giza. Kumekuwako na walio wachache sana kote chini, wakidumisha Nuru hiyo ya

Injili. Ilikuwa ni kitu gani? Masihi wadogo, wale wanaoshikilia uwakilishi wa Ufalme wa Kimasihi.

⁷⁹ Yesu hakushindwa kamwe, Yeye alifanya yale hasa aliyoagizwa kufanya, Naye alikuja kuanzisha Ufalme, na akafanya hivyo. Ufalme wa Mungu unaingia moyoni kwa nguvu za Roho Mtakatifu, unamleta Roho wa Mungu juu ya Kanisa lililotiwa mafuta kufanya ishara na maajabu kama alivyofanya Yeye, kuthibitisha ya kwamba Masihi ni Mfalme wa Ufalme Wake. Amina. Ninajisikia kupaza sauti kidogo, mimi mwenyewe, sasa.

⁸⁰ Loo, wakati kuna watu wengi sana wanaosambaza kadi, “Njoo ujiunge nasi, njoo ujiunge na *hili*, njoo ujiunge na *hili*. Tuna lililo kubwa kuliko yote, tuna *hili*, tuna la gharama kubwa kuliko yote!” Hiyo inaleta tofauti gani? Yote hayo ni upuuzi na yataangamia.

⁸¹ Lakini Ufalme wa Mungu unaimarishwa katika moyo na nafsi ya mwanadamu kwa ufunuo wa Yesu Kristo. Naye alisema, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.” Juu ya ufunuo huu, na kuwa na ufunuo unakuwa mwaminio, na kuamini ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.

⁸² Mnaona Masihi ni nini? Masihi ni Ufalme wa Mungu, waliotiwa mafuta, hao waliotiwa mafuta na Roho yeye yule aliyetiwa mafuta kwaye. Yeye. . .

⁸³ Mmoja alimwambia siku moja, “Je, wanangu wataketi mkono wa kuume na wa kushoto?”

Akasema, “Mwaweza kunywea kikombe ninyweacho Mimi? Mwaweza kubatizwa kwa ubatizo nibatizwao Mimi?”

Akasema, “Naam.”

Naye akasema, “Mtafanya hivyo. Lakini ule Ufalme, kuketi mkono wa kuume na wa kushoto sina amri kuwapa.”

⁸⁴ Kwa hiyo ilionyesha ya kwamba tungeweza kunywea kikombe kile kile cha mateso, tuitwe *Beelizebuli*, ama chochote kile, na bado tubatizwe kwa Roho yule yule aliyebatizwa naye, kwa hiyo kama aliitwa *Masihi*, na ndivyo alivyokuwa, kwa sababu alitiwa mafuta na huyo Roho Mtakatifu, na kanisa lolote lililotiwa mafuta na Roho Mtakatifu yeye yule ni Masihi mdogo, mdogo kwake, mungu mdogo. Basi siku moja wakati mwili huu utakapofufuliwa, natumaini hapo kabla, kwamba Mungu anaweza kuchukua kundi la watu ambao watadhihirisha nguvu Zake katika kila kiwango ambacho zinapaswa kuwamo.

⁸⁵ *Masihi*: “aliyetiwa Mafuta, Mfalme wa kukomboa, Mfalme.” Ninyi ni wafalme na makuhani, wafalme wa kuwaingiza, makuhani wa kumtumikia Masihi. Ishara Zake zilikuwa zifuata katika nyakati zote, zikiakisi Nuru Yake, Uwepo Wake pamoja na Ufalme Wake, watu.

⁸⁶ Sasa, usininii—si lazima ufe ili upate hii, inakubidi kufa kiroho, bali si lazima ufe kimwili. Upande wa ndani ndimo Mungu anamoingia kukutawala, Naye, anapojisukumiza Mwenyewe mbele ndani yako, usiruhusu shina lolote la uchungu, chuki, kijicho, ugomvi, ambalo lita—ambalo litamrudisha nyuma moja kwa moja tena. Ondoa tu uchoyo wote, na ushirikina, na ku—kutokuamini kwote kutoka kwako. Na kila wakati unapotoa kutokuamini kidogo, Mungu huingia mara moja, na kuchukua mamlaka, ondoa kutokuamini.

⁸⁷ Alimwambia Yoshua, “Kila mahali zitakapokanyaga nyayo za miguu yenu, hapo nimewapa ninyi.” Na usiku wa leo, tunapolingia katika ule Ufalme, Ufalme wa Mungu, tukiwaondoa wasioamini wote wa Kifilisti, na Waamori wote, na Waamaleki, na wowote wale, kuwatupilia mbali nasi namna hiyo, tunamiliki. Amina. Ninapenda hilo.

Wasema, “Siku za miujiza zimepita.”

“Ewe Mwamori, toka ndani yangu! Niliweka nyayo za miguu pale, nikamiliki.”

“Hakuna kitu kama—kama kuona maono.”

“Toka hapa, ewe Mwamaleki! Naja huko.”

⁸⁸ Haya basi, unajipenyeza utoke. Kutoka kwenye Kifungo hicho kidogo anachukua mamlaka juu ya mwili wako, akienea, Mungu akitenda kazi kupitia kwako, ndani yako, kote kukuzunguka.

⁸⁹ Si ajabu Eliya aliulaza mwili wake juu ya mtoto huyo aliyekufa naye akafufuka, ilikuwa ni Mungu katika mtu huyo. Mungu alikuwa amechukua mamlaka, alikuwa ametiwa mafuta, Yesu alisema alikuwa hivyo. Kila nabii wa Mungu katika Agano la Kale alitiwa mafuta na Roho Mtakatifu, walikuwa wametiwa, basi walikuwa Nuru ndogo. Yeye alikuwa ni Utimilifu wa Mungu, akiwa ni Masihi, hao walikuwa Masihi wadogo wakati huo, Masihi wadogo zaidi, kwa kuwa walitiwa mafuta kwa Roho yeye yule aliyetiwa mafuta naye, ila tu Yeye alikuwa Naye katika Utimilifu.

⁹⁰ Na kila mtu leo ambaye amepokea ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu ametiwa mafuta kwa Roho yeye yule ambaye Yesu wa Nazareti alitiwa naye, aliyeenda kila mahali akitenda mema na kuwaponya wagonjwa. Loo, jamani! Hilo linanifanya nijisikie vizuri kujua ya kwamba Yeye anaishi leo.

⁹¹ Kuna kitu fulani kuhusu mwanadamu, yeye ni mungu, alifanywa kuwa mungu, kusudi lake hapa duniani lilikuwa ni kuwa mungu, kuwa na mamlaka juu ya kila kitu duniani. Loo, jamani! Sasa, msiache hilo liwakwaze, kwa sababu nina Maandiko mengine zaidi yaliyoandikwa hapa chini, mnaona.

⁹² Hapa hivi majuzi usiku niliona kwenye tangazo la televisheni la mtu mwenye imani ya mawazo ya kiakili, akiweka bilauri

ya maji, kisha akasimama nyuma na kuendelea kuikazia macho bilauri hiyo ya maji mpaka akaipasua, kwa kuikazia macho tu, akaitazama bilauri hiyo ya maji, ndipo hiyo bilauri ikapasuka, nayo maji yakamwagika, kujiweka tu wakfu kiakili.

⁹³ Kwa nini? Hilo ni umbile lake, hayo ni maumbile yake. Kama anaweza kufanya hivyo, ana nguvu ndani yake, kwa mawazo ya akili, yanayoweza kuvunja bilauri ya maji, naye akiwa ni mwenye dhambi, hiyo inaonyesha ya kwamba kulikuwa na kitu kilichofanyizwa ndani ya mtu huyo. Yuko katika hali ya kuanguka—kuanguka, iliyopotoshwa, bali kama mtu huyo anaweza tu kumrudia Mungu, na kumwacha Mungu aingie ndani yake, mbona, huku nguvu hizo zikiachiliwa kwa Ufalme wa Mungu!

⁹⁴ Hakuwa na kipitishaji, alikuwa kama bunduki ya marisau, alirusha tu kwa kila njia, lakini kama roho hiyo iliyo ndani ya mtu ingeweza kuongoka, na kumweka Kristo mle ndani, ambamo ana Kipitishaji (*Kipitishaji* ni waya unaoipitisha. Amina.), na kumwacha mtu aliye na imani ile ile katika Kipitishaji cha Neno la Mungu, anaweza kuwafufua wafu, kuwatakasa wenye ukoma, kuwatoa pepo. Amina. Yeye amefanywa kama mungu, anafanana na Mungu. Hakika alifanywa, hiyo ndiyo sababu Mungu alikuwa mwanadamu, mwanadamu alikuwa Mungu, na huu ni uzao Wake, mwanadamu. Yeye anajaribu tu kumshika mtu, anajaribu kumweka mtu mkononi Mwake.

⁹⁵ Sasa, sio vipitishaji. . . Sasa, si theolojia yote iliyo kipitishaji kifaacho, mwajua, kuna theolojia nyingi ambazo ni kizuizi kutoka kwake. Tuna makanisa mengi yanayosema, “Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, pepo tu ndio wanaonena kwa lugha.” Sasa, hicho ni kizuizi, hutaki kitu kama hicho, achana nacho. Rudini kwenye Neno, Neno ndilo Kipitishaji cha Mungu. Mtu anayeamini Neno la Mungu, aliye na Neno la Mungu, anasimama juu kama majengo haya hapa wakati anapotembea juu yake. Hilo ndilo bosi, humwongoza mtu huyo, huiongoza roho, wakati akiwa mle ndani mtu anafanywa kuwa na imani kuu.

⁹⁶ Kinachofanya, nilihubiri hapa kwenye maskani hii wakati fulani uliopita juu ya *Kuonea Uzima Kiu*, ni kitu gani kinachomfanya mwanamke kutaka kutoka hapa nje na kucheza roki? Ni kitu gani kinachomfanya mvulana, mtoto tineja, kutaka kufanya hivyo? Na si hilo tu, bali babu na nyanya. Wanafanya hivyo kwa sababu gani? Ni kitu gani kinachowafanya watoke huku nje? Kwa nini watu wanataka kutenda jinsi wanavyotenda? Ni kwa sababu walifanywa wapate kuonea kiu *Kitu fulani*, na, waliumbwa waone kiu, bali waone kiu ya Mungu, nao wanajaribu kutuliza hiyo kiu takatifu kwa kumwacha ibilisi alundike juu yake kile anachokiita anasa.

⁹⁷ Kamwe, kamwe, kamwe hutairidhisha mpaka Mungu atakapoingia na kuchukua mamlaka. Unaweza kucheza dansi, unaweza kunywa pombe, unaweza kufanya uzinzi, unaweza kufanya lolote utakalo, nawe utaamka, kuumwa na kichwa, na siku moja kuzimuni. Lakini sababu ya kufanya hivyo ni kwa sababu ulifanywa katika mfano wa Mungu upate kumwonea Mungu kiu. Mungu anataka kuingia humo ndani, Mungu anataka kuruhusu Neno Lake liingie ndani yako. Na kulitumia kama Kipitishaji, Mungu alisema hivyo.

⁹⁸ Kama vile Ibrahimu, “Mungu alisema utampata mtoto.”

“Unajuaje utampata?”

“Mungu alisema hivyo.”

“Una umri wa miaka mia moja, unawezaje kumpata?”

“Mungu alisema hivyo.”

Alikuwa ametiwa mafuta. Amina. Alikuwa ametiwa mafuta, naye alikuwa na Neno, nalo hilo Neno lilikuwa limetiwa mafuta kwake, lilikuwa ni kipitishaji kinachoelekeza kwenye huyo mtoto mchanga.

⁹⁹ Mwanamume yeyote ama mwanamke, usiku wa leo, atakayechukua Neno lilo hilo la Mungu, “Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa,” uache upako, Masihi, aje juu yako, Kipitishaji hicho kitakuongoza moja kwa moja, moja kwa moja kwenye uponyaji wako, Kitakuongoza kwenye wokovu. Loo, ninakipenda tu!

¹⁰⁰ Hivyo ndivyo kitakavyofanya, maana uliumbwa upate kuona kiu, ukaumbiwa Mungu, naye ibilisi anajaribu kukupotosha, anakufanya ufikirie una wakati mzuri huku nje, aendelee kukufanya kipofu kama yeye afanyavyo, alivyowafanya Wayahudi, mpaka wakati utakapovuka mstari wa utangano, na ndipo umekwisha.

¹⁰¹ Hapo ndipo karibu taifa hili lilipo leo, wala si hili tu bali na mengine. Ulimwengu hautaliadini, Biblia ilisema katika Timotheo wa Pili 3 ya kwamba “Katika siku za mwisho hapa kwamba watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziia, wasiojizua, na wenye kuwadarau hao walio Masihi wadogo, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wenye mfano wa utauwa.”

¹⁰² Kamwe usiutarajie uinjilisti huu mkubwa, wa hali ya juu, na kadhalika, kufanya chochote, hiyo siyo njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo. “Alikuwa kwa walio Wake, walio Wake hawakumpokea.” Mnaona? Alikuwa mdogo, hakuninii. . . Mbona, aliishi mumo humo Palestina karibu maisha Yake yote, nami ningesema asilimia themanini ya watu kamwe hawakujua Yeye alikuwa mle. Lakini alitumwa kwa Kanisa, alitumwa kwa watu ambao alikuwa anaenda kuwapokea, Yeye aliwajua walio

Wake, walio Wake wanamjua, “Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu.”

¹⁰³ Msiache hilo lipite, enyi Shreveport, tafadhalini. Shikilieni hilo! “Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu kwa Neno Langu. Neno Langu, kama limefundishwa wala halitangazi jambo lile lile nililotangaza, basi ni kipitishaji kibaya.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Umasihi. Vivyo hivyo na tai aliye nalo, tunajua hilo.

¹⁰⁴ Na sasa, tunasema katika ninii ya huyo mtu. . . Huyo mtu, kabla sijaacha somo hilo, huyo mtu, yeye ni nini? Ana mkono kama wa Mungu, ana macho kama ya Mungu, ana masikio kama ya Mungu, ana mwili kama wa Mungu, aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Alipewa dunia na milki, alifanywa mungu juu ya dunia kuitawala dunia, mungu mdogo. Mungu anautawala ulimwengu, kila kitu, lakini mwanadamu alipewa dunia, kuitawala dunia, yeye alikuwa—alikuwa Masihi mdogo.

¹⁰⁵ Hivyo ndivyo alivyo usiku wa leo kama akimrudia Mungu, yeye ni Masihi mdogo, Masihi mdogo. Kama yeye. . . Kama *Masihi* linamaanisha, “Aliyetiwa Mafuta,” nawe umetiwa mafuta, basi wewe ni nani? Hiyo ni kweli kabisa, Masihi mdogo. Tunaliita hivyo kwa ajili ya Neno tu, mpaka tutakapoliendea mbele kidogo katika Maandiko. Vema.

¹⁰⁶ Uliwahi kuwazia jambo hili? Hebu niwaulize tu jambo fulani. Niangalieni kwa dakika moja. *Huu* ni mkono wangu, *hicho* ni kidole changu, *hili* ni sikio langu, *hii* ni pua yangu, lakini *mimi* ni nani? *Hicho* si *mimi*, *hicho* ni kitu changu. Mnaona? *Huu* ni mkono wangu, lakini *mimi* ninayeumiliki *huu* mkono ni nani? Huh? Mnaona, *hii* ni nyumba tu ninamoishi. Ni ninii ya namna gani. . . ?

¹⁰⁷ Vema, lazima kuwe na kitu mle ndani kinachoitwa *mimi*. *Mimi* sina budi kuwa mahali fulani, kwa sababu *huu* ni wangu. Mnaliona? *Mimi* ni mtu fulani, kwa sababu ninamiliki kitu fulani. Nina mkono, ni wangu. Vema, *mimi* ni nani ambaye *huu* ni wake? Hiyo ni roho yako. Vema, inategemea huyo ni roho wa aina gani. Yule unayesalimisha viungo vyako kwake, huyo ndiye uliye mtumwa wake.

¹⁰⁸ Halafu basi, kama unaweza kupasua bilauri ya maji kwa sababu una telepathia, dhana ya kiakili, na nguvu fulani ambazo unaweza kuziondoa kwa kuwa u mwanadamu, uweza wa nguvu za akili usioonekana, na usiojulikana, ila tu kwa duara hiyo, kama unaweza kupasua bilauri ya maji, bali kwa roho ya namna hiyo, ya kibinadamu, iliyopotoshwa, iliyolaaniwa, kwa sababu uliumbwa kwa mfano wa Mungu, unaweza kufanya nini unapomruhusu Mungu anayekuunda aingie ndani yako na kukutawala? Amina. Unaweza kutimiza kila ahadi ya Mungu. Naam, bwana. Kila ahadi Mungu aliyohidi itatimia. Vema.

¹⁰⁹ Karama ya Mungu ni Neno Lake, Mungu aliahidi, akafanya Karama, akatuma Karama, unaichukua hiyo Karama, na halafu pamoja na Neno Lake, hicho hapo Kipitishaji chako. Ukiwa na Karama ya Mungu, kama Mungu akikupa Karama ya Roho Mtakatifu (Unaamini hilo?), vema, Neno la Mungu ni Kipitishaji cha kutumia pamoja na nguvu hizo, chochote Roho Mtakatifu alichokuahidi, hicho ndicho unachoweza kufanya.

¹¹⁰ Mnaona, hicho ndicho Kitu kinacholeta Neno, Neno linatoka moja kwa moja, naye Roho Mtakatifu analifuata hilo Neno. Popote Neno linapohubiriwa, mnamwona mchungaji wenu akilihubiri, muda si muda mwajua, “*Whiu*,” Roho Mtakatifu anapitia kote jengoni. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ndiye Kipitishaji cha Neno. Neno linaenda, ama, Neno ndilo kipitishaji cha Roho, kwa sababu mahali Neno linapohubiriwa, Roho hulifuata, popote liendapo, mbona, Roho hulifuata Neno. Loo, napenda hilo! Ninapenda mafundisho mazuri ya Biblia, huku Roho Mtakatifu wa Biblia akirudi kuyathibitisha mafundisho ya Biblia.

¹¹¹ Kama Roho Mtakatifu hayathibitishi, basi nyaya zako zimeshikana, zimeungana na ardhi mahali fulani. Naam, bwana. Kama unaweza kuunganisha Neno hilo na dainamo, kitu hicho kikuu huzalisha utimilifu wa umeme, Yeye ataninii tu—Yeye atakuwashia tu maskini Waya huo, hiyo ni kweli, nao utakufanyia mambo.

¹¹² Wakati Yohana Mbatizaji alipokuja, alikuwa—alikuwa—alikuwa sehemu ya Neno, alikuwa kama Masihi mdogo. Alikuwa—alikuwa amechaguliwa na Mungu kwa Neno, alikuwa ni karama ya Mungu iliyokuja ulimwenguni. Mnaamini hilo? Isaya 40 ilisema alikuwa ni sauti ya mtu aliaye nyikani. Basi wakati alipokuja na kuchukua nafasi yake ya kulia nyikani, alikuwa kabisa haogopi pamoja nayo. Amina. Naam, bwana. Ndugu, sasa angalia vile, jinsi alivyokuwa mkuu.

¹¹³ Sasa, Mungu aliponena juu ya kuja kwa Yohana, mbona, Yeye alisema milima yote iliruka kama kondoo dume wadogo, majani yakapiga makofi, na vilima vikashushwa, na mabonde yakajazwa. Ninawazia tafsiri ya kitheolojia ya jambo hilo ilikuwa, “Enyi ndugu watakatifu, siku moja Mungu ataufungua ushoroba wa Mbinguni, ashushe ngazi ya Yakobo, ndipo kutakuwako na nabii mwenye nguvu atakayeshuka kutoka hewani, huku Malaika wasindikizaji wakija pamoja naye, wakishuka kuja duniani. Naye atashuka chini uani, papa hapa, sasa, pamoja na hekalu, mahali lilipo hekalu takatifu, na kama Kayafa ndiye kuhani mkuu, atasema, ‘Mheshimiwa, bwana, nimeshuka.’”

¹¹⁴ Loo, jamani! Ilikuwaje? Alipokuja, ilikuwa ni maskini jamaa mwenye uso uliojaa nywele za kipilipili akitoka nyikani, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, labda hakuoga

kila baada ya miezi mitatu, akitembea huko nje, amesimama matopeni kufikia magotini mwake, akasema, “Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia!” Hapo ndipo milima iliporuka kama kondoo dume wadogo, hapo ndipo majani yalipopiga makofi, hapo ndipo vilima viliposhushwa, na mabonde yakajazwa.

¹¹⁵ Kile—kile mwanadamu anachoita kikuu, Mungu anakiita kipumbavu. Nashangaa, baadhi ya ukuu wetu wa uinjilisti siku hizi, kama Mungu hauiti lundo la upumbavu, wakijaribu kumpamba mtu fulani mkubwa, aliyejaa maringo, na kila kitu. Nashangaa tu yale Mungu anayowazia juu yake. Mbona, Yeye angeninii . . .

¹¹⁶ Si, Injili hii—hii haitautikisa ulimwengu, si ya kuutikisa ulimwengu, ni ya kulitikisa Kanisa, inalitikisa Kanisa. Sasa hivi, katika miaka hii michache iliyopita, Kanisa limetikiswa kuliko lilivyowahi kutikiswa, wala ulimwengu haujui lolote kulihusu. Haikupaswa kuwatikisa walimwengu, wamekufa, kwa vyovyote vile. Huwezi kuitikisa hiyo mizoga ya kale iliyokufa huko nje, imekufa mara mbili, imeng’olewa kabisa. Unawezaje kuwatikisa?

“Vema, mimi ni mfuasi wa *Hiki-na . . .*”

Vema, endelea na uwe mshiriki wake. Unaona? Huwezi kuwatikisa.

“Vema, nyanya alifanya *hivi-na-hivi*.”

¹¹⁷ Hiyo ni kusema, haidhuru nyanya alifanya nini, Mungu anafanya nini sasa? Hii ndiyo Nuru, tembeeni ndani Yake. Nyanya aliishi katika siku zake, alikuwa sawa, bali huwezi kuyaishi maisha yake. Kwa nini usivae nguo zake basi, dada? Labda hilo kidogo lilikuwa baya sana, lakini . . . La, unataka kuchukua kanisa lake, bali hutavaa nguo zake.

¹¹⁸ Manabii wote wa kweli wa Mungu wanaikemea dhambi, wote waliotiwa mafuta hufanya hivyo. Hiyo ni kweli, wanafanya hivyo. Naye Mungu hutimiza Neno Lake kwa kila mtu, daima hulitimiza. Mungu atakuchukua . . . Hiyo ni kusema, utapokea kila ahadi kama ukipitia kwenye nyumba ya kubadilishia ya Kipentekoste.

¹¹⁹ Unajua, ukiandika hundi, hawatalipa hiyo hundi mpaka ipitie kwenye nyumba ya kubadilishia, haina budi kupitia kwenye nyu—nyumba ya kubadilishia, ndipo hiyo hundi ilipwe. Nawe unaposema ulitubu, na uko tayari kupitia kwenye nyumba ya Mungu ya kubadilishia ya Kipentekoste, Mungu atalipia kila karama aliyoahidi. Amina.

¹²⁰ Hebu jaribu Matendo 2:38 wakati mmoja, uone kama hiyo ndiyo nyumba Yake ya kubadilishia. Mnajua, Paulo alikutana na watu fulani katika Matendo 19 ambao hawakuwa wamepitia kwenye nyumba ya kubadilishia, bado. Naam. Akasema, loo,

walikuwa na furaha kuu, lakini kasema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Kasema, “Hatukujua kama kuna yeyote.”

Kasema, “Mlibatizwaje?”

Kasema, “Tumebatizwa vyema.”

Kasema, “Vipi? Kwa kitu gani?”

Kasema, “Kwa Yohana.”

Kasema, “Huo hautafaa kitu, hamna budi kupitia kwenye nyumba ya kubadilishia. Mungu tayari ameiandaa benki Yake kuzilipia ahadi hizi.”

¹²¹ Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Ahadi hizi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

¹²² Ndipo walipokutana, Matendo 2:38, Mungu aliiheshimu hiyo hundi, ikapitia kwenye nyumba ya kubadilishia, nayo hii hapa inarudi. Wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri, kumtukuza Mungu.

¹²³ Naye Mungu, wakati mwaminio anapotia sahihi jina lake kama mwaminio na kupitia katika nyumba ya Mungu ya kubadilishia ya Kipentekoste kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, Mungu atalipa kila ahadi, na chochote kile. Benki yake ni nzuri, ahadi Zake ni halisi.

¹²⁴ Kila kitu kimetiwa sahihi katika Jina la Yesu. Haiwezi kutiwa sahihi kwa njia nyingine yoyote, haitafaa kitu, Yeye hajui vyeo, Yeye anajua tu Jina. Amina. Unaamini hilo? Bila shaka, ndivyo ilivyo. Naam, bwana. Jina Lake tu ndilo jambo pekee, Yeye—Yeye alisema, “Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu.” Sasa, usiende kuweka majina manne ama matano mbalimbali mle, Yeye hajui lolote kulihusu, cheki ikirudishwa, utapata mwaliko wa bandia.

¹²⁵ Lakini wakati wowote unapopitia kwenye nyumba ya kubadilishia (Naye Mungu atakujulisha kama imepitia kwenye nyumba ya kubadilishia, au la, “Uombacho utapewa. Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo,” Yohana 15, “mtapewa.” Kweli.), ndipo mna upako, ndipo ni Masihi, Masihi wadogo, hasa, Masihi wadogo, karama ile ile iliyokuwa juu Yake.

¹²⁶ Alilitii Neno, na wakati alipokuja kulitimiza Neno, basi Mungu, Yeye alikuwa ni Masihi. Yeye alikuwa ni Ma-... Yeye alikuwa ni Yesu alipozaliwa, lakini wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu Yake baada ya ubatizo Wake, alikuwa amepata upako kwa Mungu, Mungu alikuwa ndani Yake, maana alikuja kulitimiza Neno.

¹²⁷ Unapokuja kwenye madhabahu hii, njoo hapa kulitimiza Neno la Mungu kwa mwaliko wako wa “yeyote atakaye, na aje.”

¹²⁸ Usije ukitia sahihi, “Vema, mimi, Bwana, kama utaniponya maumivu haya ya tumbo, ninaamini basi nitatumika.” Usije namna hayo. Njoo, umwambie wewe ni laghai, hufai kitu, unataka kujazwa na Roho Mtakatifu, nawe hufai hata kidogo. Hustahili chochote, unastahili kufa, na kwenda jehanamu, bali kwa sababu Yeye alikualika uje: “Naja, Bwana! Sina cha mikononi mwangu ninacholeta, ninashikilia tu kwenye msalaba Wako.” Haya basi. Yeye ataheshimu hilo basi. Kuna kidimbwi cha maji moja kwa moja kwenye orofa ya chini. Angalia kama Yeye halijali Neno Lake, Yeye sikuzote hulishughulikia, linapopitia katika nyumba Yake ya kubadilishia, bali halina budi kupitia kwenye nyumba ya kubadilishia.

¹²⁹ Mtu anaposema anamwamini Yesu, anamkubali kama Mwokozi wake binafsi, Mungu humpa kitabu cha hundi, chochote anachotaka kuomba, na hapo chini, kama tu atatia sahihi Jina la Yesu kwake, bali usishuke uende kule bila nyingine, maana haitafaa kitu. Unaona? Huna budi kupitia kwenye nyumba halisi ya kubadilishia ya Kipentekoste. Nayo inapopitia, basi hundi yako itatambuliwa, na ahadi za Mungu, Yeye daima huzilipia. Kila mmoja wa Masihi Wake wadogo wanapokea alama yao tena.

¹³⁰ Tunaishi katika siku za mwisho, kwenye wakati wa kumaliza, Wakati wa Laodikia, mmojawapo wa nyakati za giza sana zilizopata kuwapo tangu zile Zama za Giza, wakati wa kinafiki zaidi sasa hivi kuliko ilivyokuwa wakati huo, wao hawakuwa na Nuru hata kidogo. Utusitusi wa jioni ni saa ya udanganyifu, mtu yeyote anajua katika kusafiri, afadhali upunguze mwendo kidogo wakati utusitusi wa jioni unapoingia. Hiyo ni kweli? Tunapaswa kuwa na mjumbe katika huu utusitusi wa jioni. Mlijua hilo? Mungu aliahidi jambo hilo kwenye Wakati wa Laodikia.

¹³¹ Nilikuwa nikisoma katika Maandiko hivi majuzi huko juu mlimani. Nilikuwa nikisoma pale, nami... Roho Mtakatifu akaniambia, niende kwenye mti fulani na kusimama pale, Yeye alitaka kuzunguma nami. Nikasimama pale kwa nusu saa, Yeye kamwe hakusema lolote. Nikalala chini ya mwalonu huu, na kujilaza chini kabisa, nikasema, “Bwana, ulinena nami yapata maili moja hapa juu, na kusema nije hapa juu mlimani hapa kwenye Bonde hili la Mchezaji, kama nilivyoliita, Wewe utanena nami.”

¹³² Ndipo akanionyesha, wakati alipofungua Malaki, mlango wa 4. Nami nikasema... “Tazama siku inakuja, itakayowaka kama tanuru, kuwateketeza wenye kiburi,” ukitaka kuliandika, Malaki 4, Naye akasema, “itawateketeza wenye kiburi. Nao—nao wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu.” Vema, basi, Naye akasema, “Angalieni, ninawapelekea Eliya nabii kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya. Itaninii...”

Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na wana wa—wa baba, ama, mioyo ya watoto iwaelekee baba zao.”

Vema, nikasema, “Hiyo ilikuwa ni kweli, ninaamini hilo.”

¹³³ Yesu alisema wakati wanafunzi walipomwuliza hilo, walisema, “Vema, kwa nini akina nanii,” wakati alipokuwa akidai kuwa Masihi, kasema, “Kwa nini waandishi wanasema ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?”

¹³⁴ Yesu akasema, “Tayari amekuja, wala hamkumtambua.” Ndipo wakafahamu ya kwamba Yeye alinena juu ya Yohana Mbatizaji. Ni wangapi waliopata kusikia hayo? Vema, jamani, nyote mnaisoma Biblia. Yohana Mbatizaji, lakini kumbukeni, huyo hakuwa yule Eliya aliyenena habari zake, wa siku za mwisho, maana ulimwengu kamwe haukutekelezwa na ule Utawala wa Miaka Elfu kuanza.

¹³⁵ Angalieni Maandiko, angalieni usomaji wake, fungueni Malaki 4 kwa dakika moja, angalieni hapo. Sikujua hilo hapo kabla. Sijaribu kamwe kuzungumza lolote mpaka Roho Mtakatifu atakapokuja, kwanza, kulifunua. Angalieni, Malaki 4:5:

Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja ile siku iliyo kuu . . . ya BWANA: (Siku hiyo kuu, ya kuugofya ambayo Yeye ataitekeza dunia.)

Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, . . .

¹³⁶ Angalieni, mara ya kwanza Eliya alipokuja, aliigeuza mioyo ya baba zao, wale wazee, wazee wetu, mnaona, huko nyuma, wale Wayahudi wa kale, iirudie imani ya watoto waliokuwa ndio kwanza wampokee, na kuamini juu ya Masihi ajaye. “Kageuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na,” kiunganishi, kikiunganisha sentensi pamoja, “atakapokuja mara ya pili, mioyo ya watoto inawarudia baba wa Kipentekoste.” Haleluya! Haya basi.

¹³⁷ Kwa hiyo Nuru ya jioni inawezaje kuwa chochote ila kurudi kwenye Matendo tena? Kweli. Aliposema kabla haijaja siku hiyo, ambayo itaitekeza dunia kama tanuru na wenye haki watatembea juu ya majivu yao. Loo, ndugu, tunaitazamia Nuru ije, iko hapa.

¹³⁸ Basi kumbukeni, wakati huyu Eliya atakapokuja, nitawapa baadhi ya sifa zake, wakati Eliya atakapokuja, huyo ni mjumbe wa Wakati wa Kanisa la Laodikia. Tunamwona Eliya akija kabla. . . Kumbukeni, Eliya ndiye aliyepanda juu kwa gari la farasi, kamwe hakuonja mauti, Nao Ujumbe wa mjumbe huyu mkuu atakayekuja katika siku hizi za kumalizia katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati wa Kipentekoste, atakuwa Ndiye atakayelipeleka Kanisa kwenye Unyakuo. Kweli kabisa.

Yeye mwenyewe alinyakuliwa, naye atakuja pamoja na Kanisa kwenye Unyakuo.

¹³⁹ Basi kumbukeni tena, nitawapa baadhi ya maelezo ya mtu huyu, atakuwa mchukia wanawake. Hakika atakuwa, angalieni, angalieni kile alichokuwa juu ya Eliya: Yezebeli; mwangalieni Yohana: Herodia. Mnaona? Jambo lingine, yeye atapinga madhehebu kwa dhati, mwangalieni Eliya, mwangalieni Yohana, “Msiwazie kusema mioyoni mwenu, ‘Tunaye Ibrahimu baba yetu,’ Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Atayachukia madhehebu, atawachukia wanawake watovu wa uadilifu, atakuwa mtu huko nyikani, anayeishi nyikani, akitokea na Ujumbe wake, naye ataileta mioyo ya watu.

¹⁴⁰ Loo, kumekuwako na akina Eliya mia moja ambao wamekuja katika siku za mwisho. Alexander Dowie, na wengi sana ulimwenguni siku hizi wakisema wao ni Eliya, hao ni Eliya wa siku hizi. Eliya atarudi kwenye Kanisa la asili la Kipentekoste la Efeso, na kuwaletea watu Ujumbe uo huo pamoja na ishara za Masihi, Biblia ilisema hivyo, alisema, “Itakuja siku ambayo haitakuwa siku, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru.” Hiyo ni kweli?

¹⁴¹ Sasa angalieni, jua huchomoza mashariki. Sasa, hii ina... Mnasema, “Hii imekuwa ni siku ambayo ninii... Sisi ni watoto wa siku ya Injili.” Hii imekuwa ni siku ya giza kwa watoto. Nyota ya asubuhi hutangulia tu kuja wakati huo, kinyume kabisa na jinsi ilivyo hasa, kwa sababu ile Nyota ya asubuhi iliyochomoza huko nyuma, kuna Nyota ya asubuhi ambayo inatangulia kuchomoza kwa jua, na moja inayotangulia kutua kwa jua. Jua la kawaida lilikuwa likiondoka wakati ile Nyota ilipoitangulia, nayo Injili ilikuwa ndio kwanza inaingia. Sisi ni watoto wa Nuru, lakini sisi ni... ulimwengu uko gizani sasa.

¹⁴² Kanisa limepitia kwenye wakati wenye giza kuliko wote, lilipitia kwenye zile Nyakati za Giza, bali ile Nyota ya jioni, ile Nyota ya jioni ndiyo inayoitangaza Nuru. Nyota ya jioni ndiyo inayoitangulia Nuru kwa Kanisa. Kanisa limekuwa tu likiishi katika uchache, chini kabisa, kundi dogo tu. Lakini, hatimaye, siku hiyo itaninii, parapanda hiyo ya Mungu italia, nayo hiyo siku itapambazuka, Milele. Mapambazuko yaja, na huyu Roho mmoja mkuu wa Mungu atakayekuwa juu ya mtu fulani katika siku hizi za mwisho, ambayo itautangulia Ujumbe huu, itairudisha mioyo ya watoto iwaelekee baba wa Kipentekoste.

¹⁴³ Nacho Kitabu cha Matendo kiliandikwaje? Anza kukisoma. Angalieni jinsi tumekichafua kwa kila namna ya mambo yetu wenyewe ya upumbavu, bali kuna mtu atakayekuwa siku moja, Nuru, kabla ya kutua, mlango huu uliofunguliwa uliowekwa mbele ya Kanisa, angalieni mwone kama haiji katika baadhi ya siku hizi. Mungu atamtuma Eliya, hakika tu kama

ninavyosimama kwenye mimbara hii Yeye atamtuma, naye Eliya huyo atawatikisa watu warudi moja kwa moja kwenye Fundisho la asili la Kipentekoste.

¹⁴⁴ Sasa, anzieni huko Pentekoste, mwone jinsi ilivyokuwa, mwone waliyofanya, mwone kama itakuwa ni kupeana mikono, na itarudi moja kwa moja. Basi wakati Petro alipohubiri kwenye Siku ya Pentekoste kule juu, wakati wote walipojazwa na Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha zingine, watu hawa walisema, “Sasa, tufanyeje tumpate Huyu?”

¹⁴⁵ Petro akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa, Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hiyo ilikuwa Nuru ya asili ya Kipentekoste.

¹⁴⁶ Sasa, hiyo ni Nyota ya asubuhi, nayo Nyota ya jioni inapaswa kurudisha Nuru ile ile tena. Atalia kwa sauti nyikani juu ya Masihi anayekaribia, yeye pia ataonyesha—ataonyesha ishara za Masihi ajaye. Atakuwa nabii wa Mungu, mtu mashuhuri. Na ajapo, angalieni atakayofanya, Biblia inanena ya kwamba atafanya hivi.

¹⁴⁷ Pia kabla haijaja siku hiyo hapana budi kuwe na wakati wa kuingia Kanisani kutimiza yale Yesu aliyosema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sodoma, ulimwengu ungali uko katika hali ya Sodoma, sote tunajua hilo. Hiyo ni kweli, enyi kanisa? Ulimwengu uko katika hali ya Sodoma.

¹⁴⁸ Sasa angalieni, Sodoma ilipokea ujumbe wa namna gani? Walikuwa na Billy Graham wa kisasa aliyeshuka akaenda na kuwahubiria wasomi. Ni wachache tu waliotolewa nje, nao walikuwa katika aibu, na kuleta fedheha, naye huyo mke akageuka kuwa nguzo ya chumvi, akiangalia nyuma, sasa angalieni hilo.

¹⁴⁹ Malaika mmoja alisimama pamoja na Ibrahimu, yule Malaika aliyekaa na Ibrahimu, bila kujua yeye alikuwa ni nani, akidhaniwa, baada ya Yeye kusema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

Kasema, “Yuko hemani nyuma yako.”

¹⁵⁰ Biblia ilisema ilikuwa katika... alikuwa hemani nyuma ya huyo Malaika. Naye akasema, “Nitakurudia katika muhula wake. Nilikuahidi mtoto huyo mchanga, nitahakikisha kwamba utampata.”

Naye Sara akacheke moyoni mwake. Basi alipofanya hivyo, Malaika wa Bwana akasema, “Kwa nini Sara akacheke?”

¹⁵¹ Sasa, Yeye alisema hilo lingetukia *kabla* ya kuja kwa Bwana, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa

katika kuja kwa Bwana.” Mnaona, marafiki? Itaakisi Nuru ya namna ile ile ambayo ile Nyota ya asubuhi iliakisi. Naye atafanya nini? Kuwaita watoto wairudie imani ya baba zao, baba wa Kipentekoste.

¹⁵² Paulo, Sila, Yohana, Marko, Ireneo, Mtakatifu Martin, Columba, hao wote, wale wafia imani mashuhuri waliohubiri Injili hii na kuishikilia, walidumu moja kwa moja nayo kisha wakasukumwa nje, wakati maskini lile kundi kubwa la kiungwana, lilipoanza kutaka madhehebu. Mnaona katika Biblia hapo ilisema, “Matendo ya Wanikolai.” Ndipo yale yaliyokuwa matendo katika wakati mmoja wa kanisa, yakawa fundisho. Mnajua maana ya *nikao*? Nililiangalia, *nikao* maana yake ni “kuteka, kushinda.” Kushinda nini? Walei.

¹⁵³ Wakati utakatifu wote unapoingia ndani ya mtu fulani, mtu fulani pekee yake, yeye ndiye pekee aliye mtakatifu, naye ndiye, kanisa linaweza kuishi vyovyote watakavyo, wafanye maungamo kwake. Huh!

¹⁵⁴ Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya yeyote atakaye, walei na wote. Si mapenzi ya Mungu kuwa tu na mtu mtakatifu, ni Roho Mtakatifu miongoni mwa watu waliozaliwa mara ya pili, akionyesha ishara na maajabu, Kanisa lilo hilo. Nyota hiyo ya jioni itaakisi Nuru ile ile Nyota ya asubuhi iliyoakisi.

¹⁵⁵ Lakini angalieni, itakapokuja kutakuwa na wakati, Yeye alisema, “Hakutakuwa na usiku wala mchana,” ni vigumu kujua, siku yenye utusitusi, kama vile tumekuwa nayo, mvua nchini mwetu, utusitusi, “lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru.” Nuru ya jioni itakuja.

¹⁵⁶ Vema, nuru ya jioni, jua jioni ni jua lile lile linalochomoza asubuhi. Nuru ya jioni itaakisi nuru ile ile iliyoakisiwa na jua asubuhi, ni kutua tu kwa jua na kuchomoza kwa jua. Mnaliona? Sasa, tuko katika wakati wa jioni. Loo, Mungu na ashukuriwe kwa ajili ya Nuru ya jioni, hmm, hmm, ikiakisi ahadi Yake, ikiitimiza!

¹⁵⁷ Sasa, ulimwengu uko katika hali ya Sodoma. Loo, wana tai Wake! Ninayo hapa, ambapo nilihubiri juu ya hilo wakati mmoja, Nuru ya asubuhi, Nyota ya asubuhi, Ujumbe ule ule. Imekuwa jioni kwa muda mrefu sasa, ni wakati wenye utusitusi, wakati wa hatari sana. Kumbukeni, wakati wa utusitusi ndio wakati hatari sana kuliko zote, kusafiria, inakubidi kuwa mwangalifu, na hii ndiyo siku hatari sana uliyowahi kuishi. Biblia ilisema katika Mathayo 24 ya kwamba, “Itakuwa katika siku za mwisho kwamba ingewapoteza walio wateule kama yamkini.”

¹⁵⁸ Nilimsikia Billy Graham akisema hivi majuzi katika ujumbe, alisema, “Walio Wateule tayari wamedanganywa.”

¹⁵⁹ La, la, Wateule hawatadanganywa. La, la, hawatadanganyika, la. Wafuasi wa kanisa watadanganyika,

bali sio Wateule, walichaguliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, Hawawezi kudanganyika, haiwezekani, ilisema Waebrania 6, Hawatadanganyika.

¹⁶⁰ Lakini ni wakati wa hatari, na, kwa—kwa ka—kanisa katika wakati huu wa jioni, kwa sababu pale, angalieni, mngeweza . . . wataenda kanisani, na karibu wafanane kabisa na waaminio wa Kipentekoste, mtaninii . . . watapaza sauti, watacheza, watanena kwa lugha, na kadhalika, watafanana sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Lakini kumbukeni, njia pekee ambapo unajua ya kwamba uko sahihi ni kumfuata Kipitishaji, Neno, Inaleta kweli kabisa, mnaona. Uendelea na Kipitishaji, ujazwe tu Naye. Naam, bwana.

¹⁶¹ Sasa, tunaona ya kwamba kanisa hili la Laodikia, wakati wa kanisa tuliomo sasa, ukitaka kuusoma, Ufunuo mlango wa 3, tunaona ni wa aina gani . . . kilichotendeka, kile kilichotukia wakati Ujumbe huu unapopaswa kuenezwa. Kanisa lilikuwa la kilimwengu sana, na kujiundia dhehebu, mpaka wakaliunda wakamwondosha Mungu wao wenyewe kutoka kwake.

¹⁶² Andiko la kusikitisha sana nililopata kuona ni Waebrania, uh, ni Ufunuo mlango wa 3, wakati, kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia, Yesu amesimama nje ya kanisa Lake Mwenyewe, akibisha, akijaribu kurudi ndani. Kwenye kanisa la kwanza Yeye alikuwa akitembea kati ya vile vinara saba vya taa vya dhahabu, nyakati za kanisa, bali katika Laodikia Yeye alikuwa nje, akijaribu kurudi katika kanisa Lake Mwenyewe. Inaonyesha yale wakati huu umemfanyia.

¹⁶³ Wameunda madhehebu wakamtoa nje, wameunda dhehebu wakatoa Fundisho Lake nje, wakaunda dhehebu wakaaitoa Biblia Yake nje, wana kitabu cha kanuni za imani za falsafa, na kadhalika, ambacho wanakisoma na kukikubali badala yake, maungamo baridi, badala ya kumwacha Mungu aingie na kufanya Masihi wadogo kutoka kwao. Awape ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuonyesha ishara na maajabu, waliliundia dhehebu kwelikweli, wakamsukumia upande mmoja.

¹⁶⁴ Sasa, Yeye yuko nje, akitoa ombi Lake la mwisho, akijaribu kurudi tena mlangoni, “Tazama nasimama mlangoni, nabisha,” Wakati wa Kanisa la Laodikia, akijaribu kurudi kanisani Mwake Mwenyewe ambako walimsukumia nje. Hiyo si inasikitisha? Hilo ndilo jambo la kusikitisha sana ninaloweza kuwazia, la Yeye katika kanisa Lake Mwenyewe, akiyatoa maisha Yake kwa ajili ya kanisa hilo, na kufanya jinsi alivyofanya, na kutuma Nuru kanisani, na kusema Yeye alifanya hivyo, nao wakaikataa, na kumsukumia nje, wakakubali namna fulani ya kanuni ya imani, ama kitu fulani ambacho kanisa lilikuwa limebuni. Naye Huyo hapo, amesimama nje akijaribu kuingia.

¹⁶⁵ Sasa, hebu katika kufunga tu niseme jambo hili, maana tunachelewa sana, nina Maandiko kama ishirini zaidi

yaliyoandikwa hapa, bali sitayafikia, hebu niseme hivi: Mliona? Nje ya kanisa (Mnasikiliza? Semen, “Amina.”), nje ya kanisa, akijaribu kuingia, kumbukeni, wale waliokuwa ndani ya dhehebu kamwe hawakumwona Yeye. Ni wale waliokuwa nje ndio waliomwona. Walisikia mbisho, bali hawakumwona.

¹⁶⁶ Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, mtu asiyeweza, ambaye atazunguka-zunguka leo akisema, “Vema, kamwe sikuona kitu juu yake. Nilienda kule, kamwe sikuona hilo.” Mnaona, hawezi kuliona, amejitundia dhehebu sana hata hawezi kuona chochote. Lakini kama unaweza tu kuwa huru vya kutosha kutoka nje kuangalia ni Nani anayesimama huko nje akibisha, kuona ni Nani anayefanya mambo haya! Mnaona ninalomaanisha? Toka nje, nje.

¹⁶⁷ Usiwe wa kimadhehebu sana, maana ukifanya hivyo, huwezi kuona chochote, kitu pekee unachoweza kuona ni dhehebu lako. Lakini kama unaweza kutoka nje, utamwona Yesu katika utukufu Wake wote na rehema Zake, akijaribu kuingia ndani ya watu Wake. Loo, ninamtazama Yeye amesimama pale!

¹⁶⁸ Niliikuwa nikizungumza juu ya Masihi, Masihi, Masihi wadogo, wao ndio Nuru ya kanisa leo, Nuru ya ulimwengu. Yesu aliwaambia wanafunzi, “Ninyi ni Nuru ya ulimwengu.” Sasa, wewe ni mshumaa uliowekwa juu ya kilima, ambao, Nuru inayoweza kuonekana kutoka kila mahali. Sisi ndio Nuru. Kama ndivyo, tunaakisi Nuru Yake ya Masihi. Ishara ya Masihi inafuatana na hao—hao Masihi wadogo kama vile ilivyomfuata Masihi.

¹⁶⁹ Hapa wakati fulani uliopita, kanisa lenu la kupendeza hapa, ninaamini nilihubiri juu ya somo hapa *Kama Tai Ataharikishavyo Kiota Chake, Apapatikavyo Juu Ya Makinda Wake*. Ninaamini nilihubiri huo huku chini, Ndugu Jack, ama mahali fulani. [Ndugu Jack anasema, “Miaka kumi na miwili iliyopita.”—Mh.] Naam. *Tai Akitaharikisha Kiota Chake*.

¹⁷⁰ Ninapenda kumwangukia yule tai mkubwa. Mnajua nini? Baba. . . mnajua, Mungu alijiita Mwenyewe Tai. Mlijua hilo? Aliwaita manabii Wake tai. Hakika, Yeye aliwaita hivyo. Akamwambia nanii wake. . . kwamba. . . Tai huyu, Yakobo, Yeye alimwona katika hili, katika jangwa tupu, na kama vile tai ataharikishavyo kiota chake. . . Sasa, tunaona ya kwamba Yeye hujiita Mwenyewe *Tai*, pia, kwa hiyo Yeye ni Yehova-Tai. Halafu basi ana kundi la tai wadogo, *tai wadogo*, kama Masihi wadogo, tai wadogo.

¹⁷¹ Sasa, ninaweza kumwona huyo tai baba mkubwa anapotembea juu ya kiota. Anapenda kuwaangalia watoto wake. Loo, jamani, jinsi anavyopenda kuwaangalia! Wanaonekanaje? Wanafanana naye. Wao si chotara, wao si nusu mwewe, na nusu kunguru, na kitu kingine, wao ni tai. Amina.

¹⁷² Hivyo ndivyo tulivyo siku hizi, sisi ni Wamethodisti, Wabaptisti, na Waassemblies, na *Hiki-na-hiki*, na *Hiki-na-hiki*, koho, kunguru, na kadhalika, tunawezaje kuwa wana tai? Tunawezaje, wakati tunapona ishara ya Mungu ikitenda kazi miongoni mwetu, na kuiita kitu kingine? Haleluya!

¹⁷³ Anapenda kufanya hivyo, kwa sababu anajua kwamba wao ni ukoo safi. Ndivyo walivyo, wana nyama yake, wana damu yake, wana roho yake. Amina. Jinsi anavyojivunia kuwaangalia wana tai wake, wakitembea huku na huku! Amina.

¹⁷⁴ Hao wanatai wanamtazama, na kusema, “Jinsi wewe ulivyo mkuu, jinsi wewe ulivyo mkuu!” Niangalieni, loo, jamani! “Tutaruka juu moja ya siku hizi, sivyo, Papa?” Unaona? Loo, jinsi anavyopenda kuwaangalia! Wanafanana naye, wanatenda kama yeye, wao ni nyama yake, damu yake, roho yake. Amina.

¹⁷⁵ Hivyo ndivyo Kanisa la Mungu lilivyo, Wanatai Wake, Masihi Wake wadogo, wanafanana na Yeye, wanatenda kama Yeye, wanahubiri kama Yeye, wanafanya kazi alizofanya. “Mambo nifanyayo Mimi, yeye naye atayafanya; mengi kuliko haya atayafanya, maana Mimi naenda kwa Baba.” Amina. “Ishara hizi *zitaifuatana* na wanatai Wangu.” Amina. “Watafanya tu kama nifanyavyo mimi. Ikiwa Roho Yangu iko ndani yao, basi watazifanya kazi nizifanyazo, wasipozifanya hizo kazi nizifanyazo, hiyo ni kwa sababu Roho Yangu haimo ndani yao.”

¹⁷⁶ Vipi kama aliangalia chini, mmoja wa hao tai wadogo, na muda si muda wajua alikuwa na mdomo kama mwewe? Angesema, “Sasa, ngoja kidogo hapa, kuna kasoro!”

¹⁷⁷ Kunguru wa kale aliruka juu ya kiota, akaanza kusema, “*Kau, kau, kau!* Siku za miujiza zimepita. *Kau, kau, kau!* Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.”

Ha! Naweka dau Yeye angetumia tu makucha yake makubwa na kumrusha nje, naye angevunja shingo yake, mnaona, hakika kabisa. Mnaona? Naam.

“Loo, hakuna. . . Hiyo ni telepathia ya kiakili, hakuna kitu kama hayo mambo siku hizi.”

Ewe kunguru wa kimwili! Na huo ni mwili uliokufa, pia. Hivyo ndivyo ninii. . .

¹⁷⁸ Mungu anataka wanatai, anataka Masihi wadogo, anataka wanaume na wanawake walio na ishara na maajabu, waliotiwa mafuta, anataka Kanisa lililojazwa na Roho Mtakatifu. *Shooo!* Jamani! Kanisa linalomwakisi Yeye yule yule jana, leo, na hata milele! Mungu hakufa, Yeye aliuzaa tu Ufalme, akawaingiza Masihi Wake wadogo ndani Yake. Amina. Kila Neno analosema, wanaitikia, “Amina,” kwake. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Wanafanana na Yeye, wanatenda kama Yeye, wanaliadini, wana Kipitishaji kikuu kinachoenda moja kwa moja huku ishara na maajabu yakifuata; hicho ni Masihi. Masihi yu hai usiku wa

leo, Yeye hajafa, Yu hai milele. Mnaamini hilo? Yeye alisema itakuwaje?

Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata; (Hiyo ni kweli?)

Katika njia hiyo ya maji, ndiyo Nuru leo,
Kuzikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia;
Nuru za jioni zimekuja.
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

¹⁷⁹ Mwanadamu alifanywa kuwa mungu, Mungu akafanyika mwanadamu. Loo, Masihi! Yehova mkuu aliishi katika mwili wa mwanadamu, Yeye aliufanya mwili huo kama Wake kusudi aweze kufanyika mwili wa mwanadamu, Masihi mdogo, kuitawala dunia Yake na kuiongoza. Amina. “Kazi nizifanyazo Mimi, wao nao watazifanya.” Loo, napenda hilo!

¹⁸⁰ Yehova anatembea huku na huku juu ya kiti Chake cha enzi, anasema, “Hao ni wanatai Wangu. Wao ni—wao ni nyama ya nyama Yangu, na mfupa wa mfupa Wangu, wamezaliwa kwa Roho Yangu, na kuoshwa katika Damu Yangu.” Amina. “Wao ni Wangu, wao ni Wangu. Lolote ninalowaambia, wanaliadini. Kwa nini? Wao ni tai. Hivyo ndivyo walivyo, wao ni tai, kama tu vile mimi nilivyo tai. Wao ni—wao ni miungu wadogo, ambapo mimi ni Mungu mkubwa. Hiyo ni kweli. Mimi ni Yehova-Papa, wao ni watoto Wangu.” Haya basi. Kwa hiyo Yeye aliahidi mambo haya yatatukia.

¹⁸¹ Sasa, kama sisi ni watoto wa Ufalme Wake, ishara hizo zinapaswa kuwa zikijitambulisha miongoni mwetu. Hiyo ni kweli? Sasa, tunaweza kunena juu yake, na kuzungumza juu yake, na kukesha usiku kucha juu yake, lakini je, itafanikiwa? Hilo ndilo jambo linalofuata, hilo ndilo jambo linalofuata. Kama likifanikiwa, basi ni kweli. Neno la Mungu lililoahidiwa katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Hiyo ni kweli? Ninaamini hilo, nanyi je? Vema, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu basi.

¹⁸² Baba Mungu, saa ya wakati imewadia. Tunatambua ya kwamba hakuna njia kwetu ku—kupata chochote, hakuna mahali pa kwenda sasa, ila kwa Yesu pekee. Tuko—tuko katika wakati wa mwisho, tunaona mambo haya yote yakitukia: tunaona taifa letu limefilisika kabisa, tunaona ulimwengu wetu—wetu umefilisika, tunaona ukomunisti ukiingia, roho ovu inayoitwa *pazia la chuma*, tunaona moja likiinuka kule Uchina linaloitwa *pazia la mianzi*, kisha tunaona moja likitokea linaloitwa *pazia la zambarau*, *pazia la Kirumi*, likiuteka ulimwengu.

¹⁸³ Sasa, Baba Mungu, tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia kukumbuka jambo hili, ya kwamba mambo haya ni ahadi Zako, ulituhidi mambo haya wakati wa jioni. Tuna furaha sana kukuona Wewe ukilitimiza Neno Lako maishani mwetu. Tunaomba, Baba, ya kwamba utasababisha njaa na kiu. Sasa, maneno haya machache ambayo yamekatwakatwa na kuanikwa, ninaomba ya kwamba utayafanya yajulikane mioyoni mwa watu, wapate kutambua ya kwamba Mungu ni nguvu, Yeye ni *nguvu*.

¹⁸⁴ Kristo alikuwa ni Utimilifu wa Mungu, Yeye alikuwa Yehova aliyetiwa mafuta, alikuwa mwili uliotiwa mafuta na Yehova, Yesu wa Nazareti. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake, Naye alikufa apate kuitakasa jamii hii ya binadamu iliyoanguka, na kuwarudisha kuwa wana wa Mungu tena, wapate kuwa waliotiwa mafuta, waliotiwa mafuta na Roho Mtakatifu wapate kuakisi Ufalme Wake mpaka aliporudi kote katika zile nyakati saba za kanisa. Na kwenye wakati wa mwisho, tunamwona akiwa nje ya kanisa Lake Mwenyewe, akijaribu kurudi ndani.

¹⁸⁵ Lakini Yeye aliahidi ya kwamba angetuma Nuru katika siku hiyo, nasi tumeipata, Bwana. Tumeipata, na tunaona ya kwamba ni Kipitishaji sahihi, kwa sababu tuliunganisha Neno ambalo tunaamini pamoja na Mungu wa Mbinguni aliyeliahidi, na kuona ya kwamba mkondo uliofanya ishara za kwanza unarudi moja kwa moja tena na kufanya ishara zile zile za Masihi. Basi, Baba, tunajua ya kwamba Neno, tunaloliita Kipitishaji, ni la kweli, kwa sababu huzalisha kila ahadi. Tunakushukuru kwa ajili Yake, Baba.

¹⁸⁶ Tunaomba ya kwamba utawaokoa wa—wasiookoka, uwaponye wagonjwa, wajaze na Roho Mtakatifu wale wanaomtamani, na ulitie moyo Kanisa Lako. Tunapoendelea kukungojea Wewe, Bwana, katika ibada ya uponyaji, tunawakabidhi watu hawa na wote Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁸⁷ Ni kitu gani sasa? Ninaangalia saa, nami sitaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi, hatuna budi kuanza asubuhi na mapema, pia. Yeye aliahidi nini? Aliahidi ya kwamba wakati wa jioni kutakuwa Nuru. Aliahidi... Mnaweza kuona ninalomaanisha ninaposema *Masihi wadogo*? Inua mkono wako kama unaona. Kama *Masihi* linamaanisha “aliyetiwa mafuta,” Naye alikuwa Masihi kwa sababu alikuwa ametiwa mafuta kwa Utimilifu wa Mungu, basi tumetiwa mafuta, pia, kwa Roho yeye yule.

Sasa, unasema, “Kama... Unajua je umetiwa mafuta kwa Roho yeye yule?”

¹⁸⁸ Vema, Uhai ule ule, mambo yale yale aliyofanya, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya.” Yeye

alisema nini katika Yohana Mtakatifu 5:19? “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.” Masihi mdogo yeyote aliye wa kweli angekuwa na Ujumbe ule ule. Hiyo ni kweli?

¹⁸⁹ Basi kumbukeni, ni akina nani waliopokea ubatizo kwanza, ubatizo wa Roho Mtakatifu? Wayahudi. Ni akina nani waliofuata? Wasamaria. Wa mwisho walikuwa ni Mataifa. Hiyo ni kweli? Kwa sababu waliingizwa baada ya kufa, kuzikwa, na kufufuka. Nao hawakuninii... Sasa, waliupokea Ujumbe vizuri.

¹⁹⁰ Sasa angalieni, watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, sasa, watu wa Hamu na watu wa Yafethi walikuwa waone ninii... Hayo ni makabila ya duniani, yale makabila matatu ya duniani. Sasa, tunaona ya kwamba Wayahudi waliipokea ishara ya Masihi kwa Yesu, Wasamaria waliipokea kwa Yesu. Lakini sasa, siku za mwisho...

¹⁹¹ Sasa, Mataifa hawakuipokea, kwa sababu hawakuwa wakimtaalamia Masihi yeyote. Tulikuwa makafiri siku hizo, watu wetu, Waanglo-Sakson, tulikuwa makafiri, tuliabudu sanamu. Wamoabu, na kadhalika, Waamori na kadhalika, hao—hao walikuwa watu wetu.

¹⁹² Sasa, lakini sasa kwa miaka elfu mbili tumemtaalamia Masihi. Sasa, Yeye alijitambulishaje kule nyuma? Kwa kumtuma Yesu na kumtia mafuta kwa Roho Wake Mwenyewe, naye Yesu akasema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi.” Hiyo ni kweli? “Kama nikizitenda hizo kazi, aminini hizo kazi.”

¹⁹³ Sasa, kwa sababu gani? Yeye hakuungana na mashirika yao, madhehebu yao, alijitenga na hao wote, akawakemea, nao wanasema aliyavuruga makanisa, na kadhalika. Je, mngeweza kumtarajia Roho Wake kufanya lolote pungufu wakati atakapokuja tena? Atafanya jambo lile lile, maana hawezi kubadilika, ni Mungu.

¹⁹⁴ Tunaweza kubadilika, nafsi zetu za kibinadamu zinaweza kubadilika, bali Mungu hawezi kubadilika, Yeye hana budi kuwa yeye yule. Yeye hana kikomo, sisi tuna kikomo, kwa hiyo Yeye hawezi kubadilika. Kwa hiyo atakapokuja juu ya Kanisa Lake katika siku za mwisho, itakuwaje? Kundi lililovutwa nje, la watu waliotiwa mafuta kwa Roho wa Mungu, watakuwa Masihi wadogo, mnaona, watakuwa waliotiwa mafuta. Na kama Roho Wake yuko ndani yao, watafanya mambo aliyofanya, hasa kabisa. Hiyo si—hiyo si ni kweli?

¹⁹⁵ Basi ukisema... Kama unaweza kuchukua hilo, na kuunganisha Neno na dainamo, basi kama dain-... halafu kama huo mkondo ukirudi ukisema ni sawa, una muunganisho; kama ukiunganisha huko juu wala hakuna kinachotendeka,

una kizuizi mahali fulani, una waya uliokatika mahali fulani. Unaona? Lakini uunganishe na dainamo, kama mkondo ukipita, basi una kipitishaji kizuri, una kipitishaji.

¹⁹⁶ Na kama unataka kuamini ndivyo ilivyo, nitakwambia jinsi nilivyoipokea, nilikuja jinsi tu Biblia ilivyosema. Kamwe sikubadilisha kwa ajili ya dhehebu lolote, kanisa langu mwenyewe la Kibatisti lilinifukuza kwa sababu nisingemtawaza mhubiri mwanamke. Si la Kimaandiko, wala si sahihi, nami nikasema, “Afadhali mnifukuze, maana hapana shaka mtanifukuza, kwa hiyo nitaondoka tu kabla hamjafanya hivyo.” Vema.

¹⁹⁷ Ndipo mimi... Halafu inapofikia kwenye mambo haya mengi leo, mimi, nilipokuwa mvulana tu, kabla sijapata kusikia juu ya Umoja, Uwili, Miungu watatu, Miungu wanne, ama chochote walicho nacho, niliamini kulikuwa na Mungu mmoja, nami niliamini ya kwamba Jina Lake lilikuwa ni Yesu. Nami nilibatizwa katika Jina la Yesu Kristo na mhubiri wa Baptisti ya Kimishenari, maana nilimwomba afanye hivyo. Nimeihubiri tangu wakati huo.

¹⁹⁸ Hakuna Andiko katika Biblia, hebu nileteeni Andiko moja ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa katika lingine lolote, nionyesheni mahali pamoja katika Biblia ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa kwa kutumia *vyeo* vya Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Ama usome historia na uniambie, mpaka kanisa Katoliki lilipoundwa, mtu yeyote aliyepata kubatizwa kwa jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, basi nitaondoka mimbarani.

¹⁹⁹ Ni kanuni ya imani ya Katoliki, na kila mwanamume au mwanamke aliyebatizwa hivyo hajabatizwa katika Kanisa la Mungu aliye hai, wamebatizwa katika kanisa Katoliki, hiyo ndiyo kanuni yao ya imani. Nionyeshe katika Maandiko, nionyeshe kwa historia, chochote nje ya kanisa Katoliki kilichowahi kufanya hivyo.

²⁰⁰ Naye Luther akaliokota, kisha Wesley akamfuata, sisi hapa tumeshuka katika hili. Kila moja ya hayo makanisa, kufikia wakati huo lilisema, “Hamkulikana Jina Langu,” lakini ilipofika kwenye Wakati huo wa Kanisa la Thiatira, Yeye alisema, “Una jina, una *jina* ya kwamba u hai, bali umekufa.” Jambo ndilo hilo.

²⁰¹ Simaanishi ya kwamba ubatizo wa maji katika Jina la Yesu hukuokoa, lakini huo ndio ubatizo sahihi wa Kikristo, unaokolewa kwa imani, hiyo ni kweli, kwa njia ya Kristo. Hiyo ni kweli. Lakini huo ndio ubatizo sahihi, hivyo ndivyo *mtakavyobatizwa*, hivyo ndivyo hasa, jinsi ambavyo *huna budi* kubatizwa, kudumisha utaratibu wa Biblia, huna budi kubatizwa hivyo.

²⁰² Ndipo basi wakati umempokea Roho Mtakatifu, na nguvu za Mungu zinakuja juu yako, basi utafanya mambo yale yale aliyofanya Yesu, maana ni Roho Wake ndani yako. Kama

hakuna, kuna kasoro. Hiyo ni kweli. Loo, utukufu! Ninajisikia kana kwamba karibu ningeweza kunena kwa lugha sasa, mimi mwenyewe.

²⁰³ Mwajua, mara ya kwanza nilipopata kunena kwa lugha nilikuwa katika kanisa la Kibaptisti, nikihubiri. Nilikuwa nimesimama jukwaani nikihubiri kwa nguvu nilivyoweza, ndipo nikaruka moja kwa moja katikati ya marefu ya kanisa, nami nikasema maneno fulani katika lugha zisizojulikana, bila kujua niliyosema, nikaangalia pande zote, nalo kusanyiko lote likanyosha shingo zao na kuangalia pande zote. Na sasa, *Kitu fulani* kikasema kupitia kwangu, “Mimi ni—ni nyik-... Mwamba katika nchi yenye uchovu, Kimbilio wakati wa dhoruba.” Ndiyo mara ya kwanza nilipopata kunena kwa lugha.

²⁰⁴ Na, jamani, nilijua kulikuwa na kitu halisi juu yake mahali fulani, sikujua, bali niliendelea mpaka nilipokipata, nikaendelea tu kusonga mbele, nikauza yote, kila kitu, nikanunua ile Lulu kuu. Jamani, sijali, kama Biblia inasema, ni—ninaliamini, sijali ni madhehebu mangapi, ni mangapi yanayosema *hili, lile*, ama *linginelo*, Hilo ni Neno la Mungu, na ni kweli, nami ninadumu moja kwa moja Nalo, hivyo tu. Na njia pekee utakayofanya jambo hilo, ni kudumu Neno kwa Neno na Biblia.

²⁰⁵ Nilikuwa nikihubiri hivi majuzi usiku juu ya wale viumbe hai wanne, nikijaribu kuninii... Nao walikuwa, hawakuwa wanyama, kwa sababu hayo maneno katika, wao ni viumbe hai, katika Waebrania, uh, katika Ufunuo, mlango wa 4, ne—neni lililotafsiriwa ni *zoon*, z-o-o-n, ambalo linamaanisha “viumbe hai.” Katika Ufunuo 11 na Ufunuo 17 hilo ni jina lingine kabisa, nalo linamaanisha—linamaanisha “mnyama mwitu asiye fugwa,” bali huyu alikuwa ni viumbe hai.

²⁰⁶ Kwa kweli, walikuwa Makerubi, kama ilivyokuwa langoni, wakilinda mahali patakatifu. Tunawaona katika Ezekieli mlango wa kwanza, wakati Nuru ya kaharabu ya Mungu, na upinde wa mvua ulipokuwapo, na utukufu wa Mungu. Ambao tuna picha Yake, vile vile walivyoiona pale, tulikuwa na picha Yake iliyopigwa. Na Hiyo hapo, mumu humu jengoni, picha ya ile Nuru ilipigwa, kweli, jinsi hasa Ezekieli alivyoiona, Ezekieli 1:26 hadi 28, kuwaonyesha picha Yake kama tu alivyoiona, utukufu wa Mungu.

²⁰⁷ Sasa, mnaona, jicho hilo la kamera wakati mwingine linaweza kuona kitu ambacho jicho la mwanadamu haliwezi kuona. Hiyo ni kweli. Waliiona wakati wanadamu hawaioni. Lakini tunatitima sana, vipimo vyetu vya nuru, ambapo vinapaswa kuwa vipimo vitakatifu vya Nuru, vimetitima sana kwa upumbavu, na madhehebu, na kadhalika, hatuwezi kuona mbali zaidi ya pua yetu, ama ninii... namna hiyo, hatuyaoni mambo hayo huko nje.

208 Naye Roho Mtakatifu yupo hapa leo, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, Nguvu zile zile, ishara zile zile, maajabu yale yale, Mungu yeye yule, ubatizo ule ule, Roho Mtakatifu yeye yule, jambo lile lile, kila kitu ni kile kile, kwa sababu Yeye hawezi kubadilika. Amina.

Vema. Sasa, ninaamini alisema, alisambaza kadi za maombi A. Hiyo ni kweli? Kadi ya maombi... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

209 Mnaamini huko nje, enyi kanisa? Hundi haina budi kuidhinishwa vizuri, la sivyo watairudisha tena. Kwa udhahiri, si kubahatisha, bali kweli kujua ni—ni nini. Sasa, ijaze. Na sasa, Yeye tayari... .

Sasa, hebu na tumchukue mtu mgonjwa. Mtu fulani inua mkono wako kwamba u mgonjwa. Hiyo ni—hiyo ni... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

210 ...kamwe hatakanyaga hapa duniani mpaka Kanisa litakapoondoka. Ni wangapi wanaojua hilo? “Sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia wala kuwazuia hao waliokwisha kulala mauti. Parapanda ya Mungu italia, tutafufuka, tutanyakuliwa ili kumlaki Yeye hewani.” Hiyo ni kweli. Halafu anarudi kujitambulisha Mwenyewe kwa—kwa—kwa... kama Yusufu alivyowafanyia ndugu zake, wale mia na arobaini na nne elfu, bali Kanisa limenyakuliwa, na kuingia ndani. Kumbukeni, wakati Yusufu alipojitambulisha kwa ndugu zake, mke wake na wote waliokuwa kwenye ikulu, hakuna Wamataifa karibu, Yeye aliwafukuza wote.

211 Na ndivyo walivyo, wakati wa kanisa unaondoka kwenye mlango wa 3, Yohana alitwaliwa juu, akiwakilisha Kanisa. Na kuanzia hapo hadi wa 19, Yeye hayuko, ama, haonekani tena mpaka atakapokuja, akafunge ndoa pamoja na Bwana-arusi Wake. Sasa, ni kule kuondoka kwa Wayahudi kuanzia mlango wa 4 na kuendelea, matokeo ya Wayahudi.

212 Sasa, kama Kristo akija na kujionyesha Mwenyewe hai usiku wa leo... Sasa, kama nimesema kweli, kama nimesema kweli kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, na waaminio, hiyo inamaanisha Yeye ni “aliyetiwa Mafuta,” nasi tuna upako Wake, hivi si upako ule ule utafanya jambo lile lile kila wakati? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...?...

213 Nawapenda. Ndugu, ita—itakuwa imechelewa sana kuzungumza nanyi namna hiyo kwenye Hukumu, mtakapoachwa, ninawatakeni mwe tayari. Sisi ni—sisi ni... Sijui Yeye atakuja lini, lakini kama akija usiku wa leo, ninataka kuwa tayari, asipokuja mpaka juma lijalo, ninataka kuwa tayari wakati huo. Kwa hiyo ninataka kuwa tayari wakati... Kama nikilala, hilo halitanizuia, nitaamka, kwa vyovyote vile, mnaona. Lakini wakati nikiwa hapa nataka kila wakia wangu umtumikie Yeye, nami na—nataka wako ufanye hivyo, pia.

214 Sasa, mama huyu hapa, simjui. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . fanya jambo lile lile lililofanywa Sodoma. Ni wangapi wanaoamini hilo sasa kwa mioyo yenu yote? Vema. Sasa, ninaamini . . .

215 Sasa, kumbukeni, kusudi msiingize sehemu ya kibinadamu ndani yake, Mungu hufanya kazi tu kupitia mwanadamu. Ni wangapi wanaojua hilo? Mwanadamu ni naniii wa Mungu . . . Hiyo ndiyo sababu Yesu alikuwa ni Mungu. Hiyo ni kusema, Mungu alikuwa, alitenda kazi kupitia Mtu (Hiyo ni kweli?), akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Sasa, Yeye alikuwa ni Masihi, ndipo mimi na wewe tunakuwa Masihi wadogo, ama Masihi wachanga, kwa sababu tumetiwa mafuta kwa Roho yeye yule. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

216 . . . elimu ya shule ya sekondari, wala sijui chochote. Jambo pekee nijualo, nimeokoka, hilo tu ndilo nilijualo. Ninajua Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, Yeye ni Mwokozi wangu. Ninamwamini Yeye. Ninaamini Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Ninaamini Yeye alikufa, akafufuka tena, kisha akarudi katika mfano wa Roho Mtakatifu apate kulitia Kanisa mafuta. Ninaamini kila Neno la Biblia hiyo ni kweli. Mungu, nipe imani ya kulifanya lijibu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

217 . . . Nimeona likitukia tangu nilipowaacha ninyi nyote, karibu tu, labda simu ishirini, thelathini kwa siku mahali mbalimbali, na huko nyumbani. Ingeandika vitabu vizuri sana, hakika ingeandika. Lakini hatusemi lolote kulihusu, ni mara kwa mara tu kwa Kanisa. Hatulitangazi, Yesu alisema, “Usimwambie mtu.” Mnaona? Hili ni kwa ajili ya Kanisa, ni kwa ajili ya waaminio. Mnaona?

218 Sasa wewe, kama wewe ni mwaminio, sasa utaona kama Roho Mtakatifu atatenda kazi. Na kama atafanya hivyo, ni wangapi wenu watakaoamini kwa moyo wenu wote? Kama atafanya jambo lile lile alilofanya wakati alipokuwa juu ya Mtu aliyeitwa Yesu wa Nazareti, utaamini ya kwamba—ya kwamba Masihi wadogo ni ukweli? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

219 . . . ndugu, bali ni Roho Wake, mimi ni mwenye dhambi, bali ni Roho Wake ambaye hana budi kutenda kazi kupitia mahali fulani, Yeye hana budi kuwa na mtu wa kufanya kazi kupitia. Mnaona?

220 Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi. Hiyo ni kweli? Alikuwa na heri na shari zake, hasira yake ilipanda, na msononeko wake, alikuwa tu kama nilivyokuwa mimi, ama ulivyo wewe. Lakini aliomba kwa bidii, alikuwa nabii, aliomba kwa bidii na kuzifunga mbingu, akapanda moja kwa moja, akasema, “Mvua wala umande hautaanguka mpaka nitakapouagiza.” Alikuwa na jibu. Hiyo ndiyo sababu nimesimama hapa usiku wa leo mbele ya mwanamke huyu.

Mungu aliahidi, nami ninamwamini Mungu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

221 ...kuonekana katika ono. Ni wangapi walinisikia nikisimulia hayo kabla hata sijaenda Finland? Angalieni hapa kwenye hiyo mikono. Ndugu Jack alikuwa amesimama pale pale wakati lilipotukia. Mvulana mdogo aliuawa hasa, sivyo? Jinsi tu tulivyoandika katika ukurasa wa kwanza wa Biblia yetu, huyo hapo akafufuka, maskini roho hiyo ikatoka, nchi ya wafu, Mungu akaiita tena.

222 Mnaona, nguvu za akili za mtu zinazoweza kuvunja bilauri, mwenye dhambi ameumbwa kuwa hivyo, acha Mungu aingie mle, anaweza kurudi, awarudishe wafu. Mnaona? Ni ahadi Yake. Kwanza, unatafuta mapenzi ya Mungu, kisha unayafanya.

223 Vema, mnasema, "Si mapenzi ya Mungu katika kila..." Ni mapenzi ya Mungu, tayari tumeona yakifanywa. Nimeona likitendeka yapata mara tano mbalimbali, nami ninajua ni kweli.

224 Sasa, hili hapa jambo lile lile kwa njia ndogo kama Yesu alivyofanya, akanena na yule mwanamke. Hivi majuzi kulikuwa na mtu aliyekuja nyumbani kwangu, na kusimama pale, naye akasema, nikaanza kuondoka langoni, nilikuwa nikitaka kumtuma ofisini kwa Ndugu Mercier, na hao wengine, akasema, "Ndugu Branham?"

Nikasema, "Naam."

Akasema, "Waweza kunisaidia?"

225 Nikasema, "Vema, kama utaenda..." Ndipo *Kitu fulani* kikasema, "Mpeleke nyumbani." Mara tu alipoketi chini, nikasema, "Usiniambie wewe ni nani, nitakwambia." Nikaanza namna hiyo, na kumwambia yote, Roho Mtakatifu akaanza kunifunulia maisha yake yote.

Akasema, "Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli." Akasema, "Bwana, hiyo ni kweli."

226 Nami nikasema, "Ninii yako...Huishi hapa, unaishi Madison, umekuwa huko chini Evansville, Indiana, nawe ulikuwa umeingia kwenye kundi la madhehebu huko chini, sivyo?"

"Naam."

"Shule ya Biblia, ulidhani ndivyo ilivyokuwa."

Akasema, "Rehema, jamani! Unajua jina hilo?" Na kwa hiyo, wakati sisi... akatoka nje, akasema, "Aisee, sielewi hilo."

Nami nikasema, "Umewahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu?"

227 Akasema, "Sikujua jina lako mpaka yapata dakika tano hivi, kama dakika ishirini na tano zilizopita. Mtu fulani aliniambia

nilipokuwa nikipitia Louisville, nije huku, mtu jina lake Bw. Sandy.” Akasema, “Sikujua jina lako kamwe.”

Nikasema, “Vema, vema, hiyo ndiyo huduma yangu.”

Akasema, “Kama ninaelewa vizuri, Yesu alikuwa akizungumza na wanafunzi Wake na alijua kilichokuwa moyoni mwao.”

“Hiyo ni kweli.”

Akasema, “Basi huyo ni Mungu akinena nami kupitia kwako.”

Nikasema, “Jamani, unajua mengi kulihusu kuliko wengi wao ambao wameifuatilia hiyo mikutano kwa muda mrefu.” Hiyo ni kweli.

Akasema, “Vema, Mungu asifiwe, yote yamekwisha sasa basi!” Haya basi.

Mvulana ndio kwanza aingie kwa ndege kutoka Uingereza, jambo lile lile. Sasa, hili hapa, kuanzia maskanini. Hii ni kama miaka arobaini na minane yake.

Yeye ni Mungu, sivyo, Dada? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²²⁸ . . .mtu mkongwe, mzee, mama mkongwe kabisa. Ni mama yako. Ana tatizo kwenye sikio lake, naye ana matatizo, pia. Hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . .uliyo nayo mkononi mwako hapo? Vema, chukua hiyo ukaweke juu yake. Unaamini umeponywa sasa? Hebu nikuwekee mikono.

²²⁹ Baba Mungu, ninaweka mikono juu yake, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia mambo haya yatimie. Tunaomba kwa ajili ya Mungu, katika Jina la Yesu, Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . .kuamini kwamba ningerudi, ili aweze kuja huku. . .? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁰ Una shida kichwani, ni kama kipandauso. Kweli. Kimekuingiza kwenye mvurugiko wa akili. Sasa, unaugua udhaifu, inaonekana tu kama, kama tu kuchukua kamba, na kuivuta mpaka nyuzi zote karibu zikatike. Na . . .? . . .utakuwa sawa. Inez. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Nenda ukiamini. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³¹ . . .umeketi hapo ukiomba, mama uliyekunja mikono yako, una shida na mapafu yako. Hiyo ni kweli. Niliendelea kuwaona wanawake wawili, sijui huyo mwingine yuko wapi. Vema, ulimgusa Yeye. Inua mkono wako, useme, “Ninakubali uponyaji wangu.” Vema, nenda ukapone. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...hapo, pia, una ugonjwa wa sikio. Kama ataamini tu kwa moyo wake wote. Naam. Vema, pokea uponyaji wako. Nenda... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...si ndivyo ulivyo, Dada? Una matatizo ya tumbo, sivyo? Hivyo ndivyo wasiwasi wako ulivyofanya, ulikufanya ushikwe na ugonjwa wa tumbo.

²³² Unasema, “Ndugu Branham, u—ulibahatisha wasiwasi. Kwa kuwa nina wasiwasi, ulidhani nilikuwa na ugonjwa wa tumbo.” Mtu fulani aliwazia hivyo, haikuwa yeye, mtu fulani aliwazia. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...kwamba nililibahatisha. Je, ungetaka Mungu amponye shemeji yako, pia? Ungetaka? Unaamini...?...aniambie ana shida gani? Kisukari. Sasa, nenda na uamini. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...Masihi, akitembea miongoni mwetu. Yuko ndani yenu huko nje, pia. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³³ ...binti yako, wote wawili wanaugua ugonjwa wa kikoromeo. Kama unaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakupaa afya. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁴ ...matatizo mabaya, kulazwa kitandani. Nakwambia, kitu unachohitaji ni Kristo moyoni mwako. Unaona? Unahitaji kuwa Mkristo, kumkubali Kristo kama Mwokozi wako. Hiyo ni imani kubwa ndani ya mwenye dhambi, kuja karibu na karama kama hiyo, kumrehemu mama yake. Hapana shaka ila Mungu atamrehemu. Mwamini Yeye sasa hivi kwa ajili ya wokovu wako...?...Yesu Kristo akuponye. Haya basi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...shida yako ni nini? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁵ ...uliyeketi papo hapo nyuma, kidogo, umevaa koti la manjano. Jambo ndilo hilo. Vema. Nilimwona akitokea mbele yangu, nami nikaona Nuru hiyo ikining'inia hapa, kisha nikaangalia chini tena pale. Vema, Yeye alikuponya wakati huo, Dada, yote yamekwisha. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁶ ...kinywani mwako...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...ukiniangalia, na kusema, “Bwana asifiwe,” namna hiyo. Unaumwa na kinywa chako, na uso wako. Hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, Yesu anakuponya. Nenda nyumbani, na uamini.

Yeye si ni wa ajabu? Yeye ni Bwana... [Sehemu tupu kwenye kanda.]

²³⁷ ...kuamini Yeye atampa afya? Mjukuu mdogo, ana kivimbe juu ya kichwa chake. Bibi Pearson, nenda, amini kwa moyo wako wote. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁸ Wewe ni Bwana Yesu, tunakupenda. Tunajua Upako Wako uko hapa. Mbona, ni kila mahali tu, Bwana. Ninaomba ya

kwamba hawa watu watakupokea, sasa hivi, kama Mwokozi wao na kama Mponya wao. Tujalie, Bwana, kupitia Jina la Yesu.

Inamisheni vichwa vyenu kwa dakika moja tu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...?...muda mfupi uliopita...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...mstari wa maombi. Mstari wa maombi unakuja. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁹ Sasa njoo upige magoti hapa kwa dakika moja, je, utakuja? Kama unamwamini Masihi, kuamini ya *kwamba* Yesu yule alikufa na kufufuka tena, njoo hapa na usimame papa hapa mbele yangu, hapa madhabahuni kwa muda kidogo tu, na kuomba. Mungu akubariki, bwana. Ninyi wengine sasa, ninyi mnaotaka kumkubali Kristo kama Mwokozi wenu, na, njoni moja kwa moja hapa juu sasa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...?...madhabahuni.

²⁴⁰ Njoo, rafiki mwenye dhambi. Njoo, njoo kwa Kristo sasa, tumaini pekee, nafasi pekee. Nuru za jioni zinaangaza, njoo, kungali mchana, wakati unapoweza kuja. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...?...

²⁴¹ ...wote wanazama. Wamekwisha. Mchana umekwisha, usiku umeenda sana, jioni imeenda...mchana umeenda sana, usiku unaongezeka, hata Nyota ya jioni inaangaza Nuru yake. Mbona, utusitusi, wakati wa hatari!

²⁴² Usikae kitini mwako, njoo hapa juu, wewe usiye na Kristo, wewe unayetaka kumjua Yeye kama Mwokozi wako, njoo hapa na kupiga magoti wakati Yeye akiwaponya wagonjwa, Yeye huponya nafsi na mwili pia.

²⁴³ Ombeni, ninyi watu mlio na Roho Mtakatifu, wakati hawa wenye dhambi wakilia kwa kwikwi hapa madhabahuni, omba, "Mungu na akusaidie." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁴⁴ Amini. Msichana mdogo kama wewe, na mwenye wasiwasi, unaamini Yeye atakuponya huo wasiwasi? Umekuwa nao maishani mwako mwote. Unaamini Yeye atakuponya? Hebu nikuwekee tu mikono, siyo? Ninaamini Roho Mtakatifu yupo hapa, ninaamini upako upo.

Ee Yesu, maskini msichana huyu mdogo, aliyefungwa na ibilisi huyu wa mateso!

Toka ndani yake, Shetani, ninakuapisha kwa Mungu Aishiye umwache, huwezi kumzuia tena, ondoka kwake!

Nenda ukapate afya sasa. Nenda, amini kwa moyo wako wote. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Unaamini ya kwamba Mungu atauponya moyo wako, akupe afya?

Ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, apate kuponywa. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Ninaweka mikono yangu juu ya dada, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia aponywe. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁴⁵ ...waaminio humu ndani? Loo, sawa. Sasa, wakati ni—ninapoomba kwa ajili ya...Wangapi wanataka kuombewa? Inua mkono wako. Vema. Sasa, kwa nini msiwekeane mikono, ninapoomba hapa? Wekeni tu ninii yenu...Ninyi ni waaminio. Mtakatifu...Wewe ni—wewe ni Masihi kadiri alivyo mtu mwingine yeyote kama wewe ni mwaminio. Hiyo ni kweli?

²⁴⁶ “Ishara hizi zitafuata,” kitu gani? “Hao,” h-a-o, wingi, “waaminio.” Hiyo ni kweli? “Wakiweka mikono yao, *yao, yao* juu ya wagonjwa, *watapata* afya.” Hiyo ni kweli? Vema, inamisheni tu vichwa vyenu, na mwombeane sasa, wakati ninapoombea... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁴⁷ ...kanisani. Yuko wapi Ndugu L.C.? Mbona, hakika umepoteza uzito sana tangu nilipokuona miaka kadhaa iliyopita. Nilikula nyumbani kwako siku moja. Si—sijui uko hapa kwa sababu gani, unajua hilo. Lakini huenda ikawasaidia kama nikizungumza nawe kwa dakika moja tu. Sivyo? Kwa sababu ninakujua vizuri sana, huenda ikakusaidia kama ningezungumza nawe, nikisema nilikujua...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ...mimi na L.C. tulijaribu kupata yule kambare uliyenipikia, hiyo ni...?...nililithamini.

²⁴⁸ Una—una roho yako sasa. Unajua jambo fulani lilitukia wakati huo, niliishika roho yako. Umekuwa na matatizo mengi. Umekuwa hospitalini, ama kitu fulani. Umekuwa... Sasa, unaona, hiyo ni kweli. Una matatizo, umevurugikiwa tu, wasiwasi, na ugonjwa wa masikio yako, na kadhalika. Hiyo ni kweli. Wasiwasi sana, na kuvunjika moyo. Unaamini ninaweza kuondoa yote kwa Jina la Yesu Kristo? Njoo hapa.

²⁴⁹ Ewe ibilisi unayejaribu kumshikilia mwanamke huyu mtauwa, ninakupa changamoto katika Jina la Yesu Kristo, ondoka kwake! Ninamweka huru, katika Jina la Yesu Kristo.

Imekwisha, Dada. Nenda nyumbani, na uwe mzima. Roho Mtakatifu wa Mungu amekuponya.

Unatambua kwa kansa hiyo ungekufa Mungu asipokuponya. Unaamini Yeye atakuponya?

Ninaweka mikono juu ya mwanamke huyu, na kumpa changamoto ibilisi huyu, katika Jina la Yesu, atoke kwake. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Ninaweka mikono juu ya mwanamke huyu, na kumpa ibilisi huyu changamoto, katika Jina la Yesu Kristo toka ndani yake. Amina.

Hilo latosha. Hilo linalifanya kweli. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁵⁰ . . . ? . . . muda mfupi uliopita. Jambo fulani lilikupata, sivyo? Ulikuwa umesimama pale, nalo likakusisimua sana, sivyo? Hapo ndipo mgongo wako ulipoponywa. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . mbaya. Lakini Mungu ndiye Mponyaji wake, sivyo? Katika Jina la Yesu Kristo, jalia umwache, naye awe mzima. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁵¹ . . . Yesu, ninaamini Wewe ni Mwana wa Mungu, ninaamini Wewe ni Masihi. Ninaamini Wewe unatawala katika Ufalme Wako, ambao mimi ni sehemu yake kwa imani yangu katika kazi Zako zilizomalizika. Ulitufanyia ahadi hii ya kwamba “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mimi ni mwaminio, samehe kutokuamini kwangu. Mwaminio ameniwekea mikono, ninamwombea mwaminio huyo, mwaminio huyo ananiombea. Ninakubali uponyaji wangu juu ya msingi wa Neno Lako. Ninaweza kumhisi karibu kama Kipitishaji, akishuka kwenye Neno apate kuniponya.

²⁵² Sasa, Shetani, ninakupa changamoto . . . ? . . . na katika Jina la Yesu Kristo, toka wao . . . ? . . .

²⁵³ Simama kwa miguu yako sasa, kubali uponyaji wako, na umsifu Mungu kwa moyo wako wote. Utukufu! Haleluya! Sifa na ziwe kwa . . . ? . . . 

61-0117 Masihi
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org